ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nne – Tarehe 20 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1996. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1996. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny. Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1996. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Nam. 9

Zanzibar Kuathirika na Mvua za El-Nino

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Inatabiriwa kuwa kuanzia mwezi wa Septemba hadi Machi, 2010, Tanzania itaathiriwa na mvua za El - Nino. Mvua hizi pia zitaathiri Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri taarifa hii ni sahihi.

(b) Je, kama ni sahihi, Wizara yako imejiandaaje kuepusha maafa yanayotarajiwa kutokezea kutokana na mvua hizo.

(c) Je, Serikali imejiandaaje kuzilipa fidia familia zote zitakazoathirika na maafa hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.9 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Ame Ussi Juma kwanza naomba kutoa maelezo madogo yafuatayo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa wataalamu wa hali ya hewa waliochambua na kufanya tathmini ya mwenendo mzima wa misimu yetu, huko Nairobi Kenya na Harare Zimbabwe, matokeo yameonesha ongezeko la joto la maji juu ya wastani kati kati ya Bahari ya Pasifiki. Hali hii inaashiria kuwepo hali ya El-Nino ambayo inatarajiwa kuendelea hadi mwishoni mwa mwezi April, 2010. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa mvua za vuli katika maeneo ya mwambao wa Kaskazini ya Tanzania vikiwemo Visiwa vya Unguja na Pemba zinatarajiwa kuwa na mvua za wastani katika maeneo mengi ya juu na ya wastani katika maeneo machache.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa naomba uniruhusu nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Kwa taarifa ya kutabiriwa kuwepo kwa El-Nino kwa kipindi cha Septemba, 2009 hadi Machi, 2010, Tanzania ikiwemo Zanzibar ni sahihi. Hata hivyo, taarifa za utabiri huo zinaeleza kwamba ingawa mwaka huu ni mwaka wa El-Nino, haitarajiwi kuambatana na mvua kubwa kama ilivyokuwa kwa mvua za El-Nino za mwaka 1997/98. Hivyo, nguvu zake zitakuwa ni kubwa lakini sio kama zile ambazo zilizopita katika miaka hiyo niliyoitaja.

(b) Kutokana na taarifa hizo, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

- Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Kanda ya Zanzibar, kutoa matamko ya tahadhari kwa jamii yetu juu ya mwenendo wa hali ya hewa na tayari Mamlaka imeshatoa tahadhari hizo kupitia vyombo vyetu vya habari mbali mbali

na inaendelea kutoa taarifa hizo. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kuwa na tabia/utamaduni wa kuangalia au kusikiliza utabiri wa hali ya hewa unaotolewa kwenye vyombo vya habari na kuufanyaia kazi kikamilifu.

- Kuwasiliana na Kamati za Maafa za Mikoa juu ya tahadhari hizo ili na wao kuchukua hatua muafaka kwa wananchi wao ambao hasa wale wanaoishi katika maeneo yaliyo katika hatari ya kuathirika na mvua hizo iwapo zitatokezea.

- Katika utaratibu wa kushughulikia maafa kuna hatua tatu; kujitayarisha kabla maafa hayajatokea *(preparedness)*, kuchukua hatua muafaka wakati yanatokea *(response)* na kusaidia kurejesha hali za walioathirika na maafa *(recovery)*.

(c) Kutokana na utaratibu huu iwapo maafa yatatokezea kutokana na mvua za El-Nino, Serikali itasaidia kutoa huduma za kijamii kwa wale watakaoathirika. Pia Serikali tayari imeshawasiliana na Washirika wa Maendeleo, Umoja wa Mataifa juu ya kupata vifaa na madawa mbali mbali kwa tahadhari hiyo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri baada ya kusema kwamba kabla ya kufika hizo mvua za El-Nino ameshashirikiana na wafadhili wa mataifa mbali mbali ili kunusuru hili.

Lakini jengine alilozungumza Mhe. Waziri kasema kwamba yeye tayari ameshazungumza na Kamati za Maafa za Mikoa. Mhe. Spika, nataka kumthibitishia Mhe. Waziri kwamba Kamati za Maafa za Mikoa hazifanyi kazi wala hazitoi maelekezo. Kwa ushahidi niliokuwa nao kwamba hapo nyuma kuna kijana wangu pale Kikobweni aliunguliwa na moto bahati mbaya akafariki mtoto, mke na mume akaathirika vibaya, lakini ukiuliza Mkoani hakuna habari.

Hivyo Mhe. Waziri haoni asipowapa taaluma wananchi moja kwa moja yatawafika matatizo na bado patakuwa hapana msaada kutoka Kamati ya Maafa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, sikubaliani moja kwa moja na suala la Mhe. Ame Mati Wadi kwamba Kamati zetu za Maafa za Mikoa hazifanyi kazi ipasavyo. Kamati zetu zinafanya kazi ipasavyo na kimsingi kwamba kamati hizi kwanza hazikuteuliwa muda mrefu sana na mimi mwenyewe nilishiriki katika kwenda kuzizindua kamati hizi. Moja katika kazi ya kamati hizi kwanza kutathmini katika yale maeneo ambayo yana hatari ya kutokezea maafa na kupeleka taarifa mbali mbali kwa kupitia kwa Masheha.

Lakini vile vile kutokana na ombi hili la Mhe. Ame Mati Wadi, kitu tutakachokifanya tutatafuta namna ya kuwawezesha sasa Kamati zetu za Maafa kuweza kufanya vile vikao katika shehia moja kwa moja. Mhe. Spika, huwezi kusema kwamba wizara moja kwa moja ishuke kwa wananchi kwa sababu serikali tumegawana madaraka. Kuna madaraka ya serikali kuu, serikali za mikoa, serikali za wilaya, kwa hiyo kusema kwamba tushuke moja kwa moja kutoka juu tukafanye kazi mpaka chini kabisa hawa watendaji wetu itabidi sasa tuwaachishe kazi kwa sababu watakuwa hawana kazi za kufanya.

Kwa hiyo, hili suala la kusema kwamba kuna baadhi ya matukio yamejitokeza na bado hazijachukuliwa hatua, mimi kitu nitakachokiomba kwa Mhe. Mwakilishi tushirikiane pamoja katika kulifuatilia suala hili. Mhe. Spika, bado arudi tena Mhe. Mwakilishi kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa sababu Kamati ya Maafa katika ngazi ya Mkoa iko chini ya Mhe. Mkuu wa Mkoa, pengine taarifa hizi zipo lakini zinaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kama tulivyosema kwamba wizara yetu moja katika kazi zake kushughulikia masuala ya maafa na vile vile kufanya tathmini ili tuchukue hatua gani maafa yasiweze kujitokeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze Kamati ya Maafa kwa kuhakikisha kwamba inafanya shughuli zake vizuri pindi linapotokea tatizo au kutoa tahadhari kabla ya tukio kutokea.

Mhe. Spika, tunajua maafa yapo ya aina nyingi, lakini kuna yanayotabiriwa na watabiri wa hali ya hewa na mengine ni majanga tu yanayokuja bila ya kutegemea.

Kwa kuwa wananchi wetu wa Zanzibar wengi wamejenga katika mabonde ya mpungu au katika madimbwi ya maji siku za mvua huwa ni hatarishi kwa maisha yao wao na vifaa vyao. Lakini pia kwa kuwa tahadhari ikitolewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa watu wengi huchukulia kama ni maelezo ambayo hayana ukweli. Kwa kuwa watu hawa waliojenga katika maeneo haya ya

mabondeni wapo wengi, wizara ina mpango gani kupitia Kamati ya Maafa kuhakikisha kwamba wanafanya ziara katika maeneo yale na kuwapa watu taarifa mbele ya Masheha na wao wenyewe ili kuliondoa kabisa tatizo hilo lisiwafike watu wetu hao. Mwenyezi Mungu *inshaallah* ajaalie lisitokee katika eneo letu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa namna ya ufuatiliaji wake wa shughuli za serikali. Mhe. Spika, hivi ndivyo inavyotakiwa Waheshimiwa Wawakilishi wawe watchdog. Watchdog maana yake wanaikagua serikali shughuli gani inafanya, wakati gani inafanya shughuli wanaipongeza na wakati haifanyi wanaiambia. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa kufuatilia utendaji wa shughuli zetu.

Mhe. Spika, nikimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, ni kweli kwamba wananchi wetu wamekuwa wakaidi. Serikali yetu tunajitahidi kuwaelimisha wananchi na wakati mwengine wanahisi kwamba labda tunakwenda kuwasumbua katika maeneo yao. Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi nimeshafanya ziara katika maeneo mbali mbali nikatoa tahadhari kwamba watu waache kujenga katika mabonde ya mpunga lakini pia katika yale maeneo yanayopita maji hasa wakati wa mvua.

Katika maeneo haya ya mabonde ya mpunga, maafa sio kwa mvua tu zitakapotokezea, lakini maafa yanakuja hata kusababisha njaa katika nchi. Kwa sababu utakapojenga katika maeneo ya mabonde ya mpunga ina maana wale wakulima waliokuwa wanalima pale itabidi sasa wakatafute kibarua chengine wakati hicho kibarua chenyewe hawana. Lakini katika yale maeneo wanayojenga watu ambayo kuna mabonde yanakaa maji wakati wa mvua serikali imeshatoa tahadhari sana.

Mhe. Spika, nitatoa mfano mdogo, Sebleni pale serikali ilifika pahala mpaka ikawahamisha watu ikawapa viwanja sehemu nyengine. Vile viwanja sehemu nyengine wamejenga lakini na pale wamerejea tena kujenga vile vile. Kwa hiyo, serikali inajitahidi lakini wakati mwengine wananchi wetu wanakuwa wakaidi.

Sasa kutokana na hali ya hewa ilivyobadilika duniani sasa hivi, kuna mikutano mbali mbali ya kimataifa ambayo inafanyika inazungumzia hali mbaya ya hewa duniani. Jana Mhe. Spika, katika hii jitihada tunayoifanya kama wananchi wetu walikuwa wanaangalia taarifa zetu za habari mbali mbali, wenzetu wa Idara ya Hali ya Hewa walikuwa wanatoa namna gani athari ilivyoanza kwa Tanzania yenyewe, kuna baadhi ya visiwa vimeshaanza kufukiwa na maji. Juzi

nilivyosema hapa tukija tukiamka tutajikuta hatupo Waheshimiwa Wawakilishi walicheka lakini haya ndio mambo yenyewe yalivyo.

Kuna baadhi ya mafungu katika maeneo ya Mafia sasa hivi hayaonekani yameshazama, kwa hiyo hii inaonesha kwamba kina cha bahari kinazidi kukua. Mhe. Spika, sisi nchi yetu ni ndogo, sasa haya maeneo yanayokaa maji, yanayopita maji bado tunaendelea kutoa tahadhari wananchi wetu wasiyatumie katika ujenzi hasa kutokana na mvua za sasa hivi hazina dhamana. Sasa hivi wakati wa Kiangazi basi linaweza likaja mvua hilo halina idadi.

Kwa hiyo Mhe. Spika, nakubaliana na hoja za Mhe. Mwakilishi kwamba sisi serikali tutaendelea kutoa taaluma kwa wananchi wetu lakini pia na Waheshimiwa Wawakilishi na wao katika maeneo yao wajitahidi kushirikiana na madiwani na masheha katika kuhakikisha kwamba katika maeneo ya hatari wananchi wasiweze kuyatumia kwa ujenzi.

Nam. 33

Ujenzi wa Jengo Jipya la Wizara ya Fedha – Pemba

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Wizara ya Fedha na Uchumi, Pemba imeanza kujenga jengo lake jipya Tibirinzi. Ujenzi wa jengo hilo, ulioanza Julai 2009, umeshachukua wiki 12 na hatua iliyofikiwa ni kutandikwa kwa jamvi la chini.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kwamba Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba haikushirikishwa katika ujenzi huo.

(b) Je, Mhe. Waziri unajua kwamba ardhi ya eneo ilipojengwa misingi ya jengo hilo inatoa maji kutoka chini ya ardhi na Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo Kampuni ya *ELECTRI PLAN LTD* ya Dar es Salaam ameshakimbia.

(c) Ujenzi wa jengo hilo, kuanzia Septemba 2009 hadi kukamilika kwake umebakiwa na wiki 35 tu. Je, kutokana na muda huo, upo uwezekano ujenzi huo ukakamilishwa kwa wakati.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kufanya marekebisho katika kifungu (b) cha swali lake kwamba Mkandarasi aliyeshinda Zabuni na kubarikiwa kazi ya ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Pemba ni Kampuni ya *Johnson Construction Company Limited* na sio Kampuni ya *Electric Plan Ltd* ya Dar es Salaam kama ilivyonukuliwa na Mhe. Mwakilishi. Baada ya marekebisho hayo sasa naomba kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Makao Makuu ya Wizara ya Fedha na Uchumi inayo mashirikiano mazuri sana na Afisi yake iliyoko Pemba katika mambo yote ya kuendesha wizara na hususan hili la ujenzi wa jengo lake jipya. Mashirikiano hayo kwa ujenzi huu yalihusisha tangu hatua za mwanzo ikiwa ni pamoja na utafutaji wa kiwanja, mahitaji ya Afisi zinazotarajiwa kuwemo katika jengo jipya, mchakato wa kumpata mshauri na hatimae kumpata mjenzi mwenyewe. Aidha, Afisi ya Wizara ya Pemba inashiriki kikamilifu katika vikao vya pamoja baina ya Wizara, Mjenzi na Mshauri kwa madhumuni ya kufanya tathmini ya maendeleo ya ujenzi *(site meetings).* Aidha, Afisi ya Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba kwa kushirikiana na Mkandarasi imefuatilia upatikanaji wa huduma muhimu katika kufanikisha ujenzi unaoendelea ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za maji, umeme na eneo la kutunzia vifaa.

(b) Mkandarasi Mkuu *(Main contractor)* wa ujenzi wa jengo la Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba kama nilivyosema Kampuni ya *Johnson Construction Co. Ltd* na Mshauri Mkuu ambaye ni *K &M Archplan Ltd.* Kwa nyakati tofauti, mkandarasi huwa anaingia mikataba na Kampuni nyengine *(Sub-Contractors)* kwa kazi maalum. Mhe. Spika, ni kweli kwamba ardhi ya eneo ilipojengwa misingi ya jengo hili la Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba ina mahitaji maalum kutokana na ardhi yake kuwa na maji kwa muda mwingi. Kwa kuzingatia hilo, mkandarasi aliiajiri Kampuni ya *KRYTON Ltd* ya Dar es Salaam kama *sub-contrator* kufanya kazi ya kuzuia maji hayo *(Water proofing).*

Kwa hiyo *sub-contractor* huyu alipomaliza kazi yake akaondoka hakukimbia kwa kushindwa kazi. Mhe. Spika, kazi imemalizika na msingi umekamilika, mimi mwenyewe

nilikuwepo *site* juzi nimeshuhudia na kwa kweli anahitaji kupewa pongezi kazi ni nzuri kabisa. Ujenzi unaendelea kwa kasi sana na umezingatia mahitaji maalum ya eneo hilo na kuchukua tahadhari na mapema.

Kama nilivyosema kitu cha kufurahisha zaidi ni kwamba hii Kampuni ya Johnson imemuajiri site engineer mzalendo ambaye kama mzalendo basi mbali ya kutimiza wajibu wake lakini anatusaidia sana katika kusimamia shughuli nzima ya ujenzi hapo Tibirinzi.

Kampuni ya *Electric Plan* ya Dar es Salaam si mjenzi bali anashughulika na kazi ya uwekaji wa umeme katika jengo hilo na bado kampuni hiyo ipo kwa vile shughuli zake hazijamalizika. Kwa mantiki hii, hakuna kampuni iliyoondoka kwa kushindwa kazi.

(c) Ni kweli kwamba kuanzia mwezi wa Septemba, 2009 ujenzi huo utakuwa umebakiwa na kipindi cha wiki 35 hadi kukamilika kwake kwa mujibu wa makubaliano. Napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako Mhe. Spika, kwamba muda huo unatosha kukamilisha kazi iliyosalia. Ni matarajio yetu kwamba ujenzi huo utakamilika kwa wakati mwezi April, 2010.

Nam. 62

Matengenezo ya Bustani ya Forodhani – Zanzibar

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na Shirika la Agakhan kwa matengenezo mazuri ya Bustani ya Forodhani. Wananchi, watoto wamepata eneo zuri na safi la mapumziko na kupata huduma za vyakula na vinywaji mbali mbali kwa siku zote. Aidha, bustani imetoa haiba nzuri kwa mji wetu mkongwe na wageni wamezidi kuvutiwa na eneo hilo.

(a) Tumesikia katika vyombo vya habari mnamo mwezi wa Agosti, 2009 kuwa watu watatu (3) walikamatwa wakiharibu bustani hiyo. Je, jambo hili ni kweli.

(b) Ni uharibifu gani walioufanya na adhabu gani wamepewa kisheria.

(c) Je, kwa wale wafanyabiashara ni kiasi gani cha fedha wanachochangia kwa mwezi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali kwanza namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuipongeza serikali kupitia Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Pamoja na taasisi ya *Agakhan Foundation* kwa kuitengeneza Bustani ya Forodhani na kuifanya nzuri sana na ya kileo na wageni wengi kupenda kutembelea eneo hilo.

a) Ni kweli katika mwezi wa Agosti, 2009 walikamatwa watu watatu wakiharibu bustani hiyo.

b) Uharibifu waliofanya ni kutapakaza maji ya chumvi wakiwa wanatoka kukoga pwani katika bustani na sehemu za vibaraza vinavyokaliwa na watu na kufanya hivyo ni makosa kwa mujibu wa taratibu za bustani ya Forodhani na vile vile inachangia kuharibu majani kutokana na maji ya chumvi na vibaraza viliopo. Wananchi waliokamatwa walifikishwa katika vyombo vya sheria na waliachiwa baada ya kupewa onyo kali.

c) Wafanyabiashara wa eneo hilo watalipa viwango mbali mbali vya malipo kulingana na aina ya biashara na ukubwa wa nafasi watakayotumia. Kwa mfano :-

    1. Vibanda vya biashara *(kiosks)* - Tsh. 1,500,000 hadi 2,000,000/= kwa mwezi.

    2. Huduma za ukodishaji vyoo - Tsh. 320,000/= kwa mwezi.

    3. Huduma za eneo la kucheza watoto - Tsh. 400,000/= kwa mwezi.

    4. Biashara za vyakula chipsi/kuku – Tsh. 90,000/= kwa mwezi.

    5. Biashara ya *juice* ya miwa – Tsh. 45,000/= kwa mwezi.

6. Biashara ya genderi, muhogo wa kuchoma – Tsh. 30,000/= kwa mwezi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kupitia Wizara yake, Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na Manispaa yetu kwa kutujengea bustani nzuri ambayo tunaamini kwamba wageni wetu wengi wamevutiwa katika eneo hili.

Lakini pia Mhe. Spika, niseme tu kwamba pamoja na kazi hiyo nzuri ambayo ina ulinzi mzuri kuhakikisha kwamba inakua siku hadi siku katika mandhari nzuri isiharibike.

Kwa kuwa kuimarisha mji wetu hutegemewa sana kupata bustani mbali mbali. Kwa kuwa mji wetu huu bado una maeneo mazuri ambayo huwa ni kivutio kwa wageni hata na wazalia wa nchi hii kwa ajili ya mapumziko na kufanya biashara zao kupata tija zao.

Mhe. Spika, kwa kuwa tuna eneo kubwa la bwawa la Bwawani ambalo ni la muda mrefu na linakuwa katika mazingira machafu na kusababisha mbu na maficho ya majambazi wakati mwengine. Hivyo, Wizara kupitia Manispaa ina mpango gani katika tafiti zao kuhakikisha kwamba eneo lile linafanyiwa kazi na kuwekwa biashara ambazo zitakuwa ni kivutio kwa vijana wetu na watu wetu wote, hata wageni wanaopita pale ni pahala ambapo ni mandhari nzuri katika mji wetu.

Mhe. Spika: Hili swali ni zuri kweli kweli, lakini hebu turudi kwenye bustani ya Forodhani. Sasa tufanye utaratibu uliulizie kwenye swali la msingi. *(Kicheko)*

Malipo ya Kodi kwa Nyumba za Serikali

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za ujenzi wa nyumba na hatimaye kufikiria haja ya kuwakodisha wananchi. Hali hii sio tu inawasaidia wananchi wanyonge, lakini pia inajenga imani na ukaribu kwa wananchi na Serikali yao.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna vigezo gani vinavyotumika katika ukodishaji wa nyumba hizo kwa wananchi ?

(b) Kuna sababu zipi zinazopelekea nyumba hizo kukodishwa bila ya kulipwa kodi kwa zaidi ya miaka miwili ?

(c) Kwa kuzingatia mahitaji na shida za wananchi wetu, Je, Wizara haifikirii kwamba ipo haja ya kukatisha kodi kwa wadaiwa sugu na hatimaye kuwakodisha wananchi wengine wenye moyo wa kulipa kodi kwa wakati ?

(d) Je, Wizara haina nyumba yoyote iliyojengwa na kukodishwa Tanzania Bara, na Je, kwa nini Serikali haijafikiria haja hii mpaka leo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 lenye vifungu (a), (b), (c), na (d) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, vigezo vinavyotumika katika ukodishaji wa Nyumba za Serikali, kwanza ni kwa mwombaji kuwa na mahitaji ya makaazi, na vile vile kwa mwombaji kupeleka maombi yake katika Idara husika ya Nyumba na Maendeleo ya Mkaazi kwa ajili ya kuzingatiwa. Kimsingi lengo la serikali ni kuwasaidia wananchi wake wote kuwapatia makaazi yalio bora. Lakini kutokana na wingi wa maombi inakuwa vigumu kwa kila mwombaji kuweza kumpatia nafasi katika nyumba zilizopo.

(b) Mhe. Spika, kimsingi kila anayekodishwa Nyumba za Serikali hutakiwa kufuata taratibu za ukodishaji likiwemo suala la kulipa kodi kwa wakati. Ni kweli inatokezea baadhi ya wapangaji hukaa muda mrefu bila ya kulipa kodi na inapotokezea hivyo basi hatua za kumfuatilia mpangaji huyo huchukuliwa, ikiwa ni pamoja na kumwita Afisini kumkumbusha, kumuandikia barua ya ukumbusho wa deni, kumpa tahadhari ya kushtakiwa na ikibidi kumshtaki katika Bodi ya Kudhibiti kodi za nyumba. Hatua zote hizo huchukuliwa kwa lengo zuri tu la kuhakikisha wapangaji wanalipa kodi zao bila ya usumbufu.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kuwa wananchi wengi wana shida za makaazi. Lakini vile vile kwa kuzingatia misingi ya Sheria na Utawala Bora inakuwa sio busara kuwakatisha upangaji wadaiwa sugu na kuwakodisha wengine. Ni vyema kwa yule aliyekiuka taratibu za upangaji kumfikisha katika Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na baadaye ikithibiti kosa ndio kumuondoshea upangaji wake, ili haki itendeke na kuepusha malalamiko yanayoweza kutokea.

(d) Mhe. Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu za wizara, bado wizara haina nyumba iliyojengwa au kukodishwa Tanzania Bara. Lakini

kunauwezekano wa baadhi ya Taasisi za SMZ kuwa na majengo Tanzania Bara ingawa taarifa za Afisi hizo hatunazo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri aliyokuwa kayafafanua hapa, naomba kumuuliza swali moja tu.

Je, anafikiria nini kilichosababisha msajili wa nyumba Tanzania Bara wa nyumba za maendeleo, kuwa nyumba zile zinakodishwa na mapato yanayopatikana yanasaidia katika kuboresha masuala mbali mbali, yakiwemo makaro na kwa wale wanaotumia matumizi mabaya ya kuni kuziweka katika hali ya usalama. Je, ananiambia nini kulingana na utekelezaji wa msajili wake wa nyumba hapa Zanzibar ili zipate maendeleo kama haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, bahati mbaya sielewi ufanisi uliopatikana kwa nyumba za serikali kule Tanzania Bara, lakini najua kwa hapa kwetu. Kwanza tunawajibika wote wale ambao tumepewa nyumba za serikali, ili kuhakikisha kwamba nyumba zile tunazitunza. Kwa sababu ndio tunazitumia, tunakaa na watoto wetu, tunazaa na tunajukuu. Kwa hivyo, ni lazima tuzitunze.

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunajaribu kukemea, kuna baadhi ya watu huwa wanatwanga mle, tunakemea hilo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tuendelee sote kwa pamoja kuona kwamba tunazitunza nyumba hizi ikiwa ni zetu, kwa sababu serikali hii ni yetu na nyumba zile ni zetu.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwanza nieleze kwamba kwa Zanzibar hatuna msajili wa nyumba, bali tuna Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Ufanisi tunao.tena wa hali ya juu, kwa maana ya Baraza lako tukufu hili limepitisha sera ya taifa ya nyumba kwa kuweka mwelekeo thabiti juu ya namna bora ya kusimamia nyumba ambazo zinamilikiwa na serikali, kwa maana ya *Government House Stock*.

Mhe. Spika, tayari katika taratibu hizo tulikubaliana kwamba baadhi ya nyumba hizo ambazo tunapata tabu katika utunzaji wake, kutokana na pengine kutokuwa na uwezo wananchi wa kulipa kodi kwa wakati na kadhalika, kuanza utaratibu wa kuuza. Hilo tayari limeshaanza kwa nyumba za vijijini na hatimaye kuelekea katika miji mikuu kwamba baadhi ya nyumba zile zitaendelea kubaki mikononi mwa serikali.

Mhe. Spika, nyumba ambazo zimetangaziwa rasmi kwamba zina umuhimu wa kihistoria, kitamaduni na zilizokuwa zimetiwa kwenye gazeti rasmi la serikali

zitaendelea kubaki mikononi mwa serikali, zinazotumika na serikali zitaendelea kuwemo mikononi mwa serikali na nyengine zilizokuwa na umuhimu kwa serikali zitaendelea kubaki hivyo, ili utunzaji wake na usimamizi wake uwe mzuri zaidi.

Mhe. Spika, taratibu za uuzaji wa nyumba za vijijini tayari kama tulivyokubaliana na kama nilivyosema awali Mhe. Spika, umeshaanza.

Nam. 24

Kuimarishwa Uwanja wa Michezo Gombani – Pemba

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Katika hatua ya kuimarisha Uwanja wa michezo wa Gombani Pemba hatua za awali za matayarisho ya upelekaji wa umeme mkubwa katika uwanja huo kwa lengo la ufungaji wa taa zimeanza. Kazi hiyo inakadiriwa kugharimu Tshs. 33,000,000/=, ambazo hadi kufikia Juni 2009 zishalipwa Tshs. 18,000,000/= kwa awamu ya kwanza.

(a) Je, Mhe. Waziri, fedha hizi zinalipwa na Serikali au na Washirika wa Maendeleo ?

(b) Kazi ya uwekaji wa taa hizo inafanywa na Kampuni gani au Serikali ?

(c) Je, kazi hiyo tangu kuanza kwake hadi kumaliza itachukua muda gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima katika kikao hiki.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kazi ya upelekaji wa umeme mkubwa katika Uwanja wa Gombani kwa lengo la ufungaji wa taa umegharimu Tshs. 33,000,000/=. Hadi kufikia mwezi wa Oktoba, 2009 zimeshalipwa Tshs. 24,000,000/=, yaani milioni 6 zaidi kuliko zile alizouliza Mhe. Mwakilishi kwa mikupuo 3. Kazi kwa asilimia kubwa imeshakamilika ila bado kuunganishwa "*line*" kubwa kutoka katika *transforma* hapo nje ya Uwanja wa Gombani.

(a) Mhe. Spika, naomba kumjulisha Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kuwa fedha hizi zote zimelipwa kutoka mfuko wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(b) Kazi ya uwekezaji wa taa za uwanja na sio umeme, itafanywa kwa msaada wa Mfadhili, yaani Jumuiya ya Sheikh Al-Youseif. Kwa kuwa kazi hiyo ya uwekaji wa taa hizo unahitaji utaalamu ili kuondosha kivuli wakati wa kucheza, basi mfungaji wa taa hizo atateuliwa na yeye Mfadhili mwenyewe. Tayari mfungaji huyo alishafanya ziara ya awali ya kuangalia na kutazama sehemu za minara zitakapofungwa taa hizo.

(c) Hakuna muda maalum uliowekwa kumaliza kazi ya uwekaji wa taa, wala makubaliano na mwekaji wa taa hizo. Mara tu itakapomalizika kazi ya uungaji wa *line* kwenye *transforma* itakayokuwepo hapo nje, wizara itawasiliana na Jumuiya ya Sheikh Al-Youseif kuanza ufungaji wa taa hizo mara moja.

Hivi sasa tunasubiri fedha za mwisho, Sh. 900,000/= kulipa Shirika la Umeme yaani *ZECO* ili wakamilishe kazi hiyo, kwa kuwa wataalamu wa Jumuia hiyo ya Sheikh Al-Youseif wako hapa Zanzibar kwa ajili ya kufunga taa hizo katika ukumbi mpya wa Baraza la Wawakilishi ambalo tunaamini utapendezeshwa na taa hizo za usiku, basi tutatumia muda huo huo wa kuwatumia wataalamu hao kutufungia taa hizo katika Uwanja wa Gombani, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa hatua za kufunga mataa kwenye Uwanja wa Gombani zinaonesha hali nzuri, kwa pesa zilizobakia naamini hazitofikia muda mkubwa zitamalizika.

Mhe. Spika, katika hilo ilikuwa sio taa pekee yake zitakazoufanya Uwanja wa Gombani uwe unachezeka vizuri, lakini tulisikia pia zitawekwa nyasi bandia. Taa imefikia hatua hiyo je, nyasi bandia zimefikia hatua gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa ni kwenye taa ndio maana sikugusia maendeleo mengine ambayo yamefanywa katika Uwanja wa Gombani. Pamoja na hayo maendeleo mengine, hivi sasa tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshalipa *cheque* ya dola 120,000 kama tulivyokuwa tunatakiwa ni zaidi ya Shs. 150,000/= hizo, kama tulivyokuwa tunatakiwa na *FIFA* katika mpango na mradi wao wa kutusaidia katika nyasi za bandia. Jumla ya fedha zote zinazogharimu nyasi hizo ni kama dola 400,000. Mchango wetu sisi ni dola

120,000 tayari fedha hizo zimeshawasilishwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi sasa tunasubiri nyasi hizo kufika hapa Zanzibar. Tunavyoambiwa zitakuwa ni nyingi sana ni zaidi ya kontena 8 kwa sababu zinatandazwa na kusambazwa na mambo mengineyo.

Pia kuna mambo mengine ambayo yamefanyika ambayo hatukuyataja ni kupaka rangi uwanja mzima wa Gombani, pamoja na kutengeneza ile *running track* ya pale Gombani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamadunina Michezo kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu lake la Mhe. Naibu Waziri kwa swali la nyongeza aliloulizwa, alisema kwamba pamoja na kuulizwa hapari ya ujenzi, lakini pia aliyoulizwa mengineyo vile vile kayajibu, namshukuru kayajibu vizuri. Kwa hivyo, na mimi nitapata kuuliza hapa hapa.

Mhe. Spika, nia na madhumuni ni kwamba kukuza wana michezo wetu katika fani mbali mbali za michezo katika nchi yetu, kwa mpira wa miguu, riadha, basketball, netball na michezo mingine yote. Kwa bahati nzuri Mhe. Spika, Chama cha Mpira *ZFA* Wilaya ya Mjini huwa kila mwaka kinaandaa mashindano makubwa ya kusherehekea Mapinduzi *CUP* na sherehe hizi hukutanisha timu mbali mbali za Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa mfano, Simba, Yanga, Mtibwa, Jamhuri kwa Zanzibar, Miembeni na nyinginezo. Kwa kuwa mashindano haya huwa ni kivutio kwa wananchi wetu na kiwanja ambacho tunakitegemea huwenda kikatumika kwa muda huu ni hichi hichi.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wenzetu hawa *ZFA* Wilaya ya Mjini hubeba mzigo huu mkubwa na kuitangaza nchi yetu kutokana na mashindano hayo, ina mpango gani wa kuwatafutia wadhamili ili mashindano hayo yaende vizuri zaidi ?

(b) Katika kukuza hiyo hiyo michezo Mhe. Spika, katika mikoa ya Tanzania kuna mashindano ya Kopa Koka Kola ambayo vijana wetu wa Mjini Magharibi ni mabigwa wa Tanzania nzima na kwa upande wa riadha vijana wa Mkoa wa Mjini Magharibi ni mabigwa wa Tanzania katika mashindano hayo. Kwa kuwa kulikuwa kuna ahadi kwamba vijana hawa watakwenda kumkabidhi makombe Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa bahati ilifutika ile riadha. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri. Je, suala hili bado lipo, ili tuwape changamoto vijana wetu na hamasa zaidi ili wafanye vizuri mwakani.

Mhe. Spika: Mheshimiwa wangu, Mhe. Ali Suleiman Ali, hebu turudi hapa Uwanga wa Gombani. Mhe. Naibu Waziri anataka akusaidie, lakini hapana, hebu twende kwa utaratibu. Maana hili swali linahusu Uwanja wa Gombani, tena lilikuwa linahusu taa. Lakini kwa sababu ya maendeleo ya uwanja ndio nikaruhusu hilo la nyasi, kwa sababu uwanja wenyewe ndio ule ule wa Gombani. Angeutaja Uwanja wa Mau, hapo sasa ingekuwa ni uwanja mwengine sasa. Tuendelee na maswali mengine sasa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema katika ujenzi wa Uwanja wa Gombani itakuwemo pamoja na *running track*. Swali langu je, hii *running track* itajengwa kwa mchanga, fusi, saruji, lami au itatiwa *tartan*?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza naomba kumjulisha kwamba hiyo *running track*, tayari imeshatiwa na hivi sasa ipo na ilitengenezwa kwa mchanganyiko wa lami nyepesi na mchanga, ambapo kazi hiyo ilifanywa na ndugu zetu wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ahsante sana.

Nam. 34

Ujenzi wa Jengo la Radio Jamii – Micheweni

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga jengo la Radio Jamii, Micheweni Pemba kwa lengo la kutoa ajira kwa wananchi wa Micheweni na vitongoji vya jirani, kutoa taaluma kwa wananchi hao na kuwaunganisha na jamii jengine kimawasiliano.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inao mpango wa kujenga majengo mengine ya radio jamii katika maeneo mengine, Unguja na Pemba.

(b) Jengo hilo la Micheweni mpaka kumalizika kwake litagharimu kiasi gani. Aidha vifaa vya radio hiyo vitagharimu kiasi gani.

(c) Inaelezwa kuwa kuna mpango wa kujengwa nyumba za wafanyakazi ni lini na ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kwanza nitoe taarifa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikujenga jengo la Radio Jamii, Micheweni Pemba kwa lengo la kutoa ajira kwa wananchi wa Micheweni na Vitongoji vya jirani kama Mheshimiwa alivyoeleza katika swali lake la msingi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kulifanya eneo la Micheweni kuwa ni kijiji kipya cha millenia katika mpango wa millenia wa ulimwengu mzima. Sababu zote za maamuzi hayo zinafahamika, na kwa nini eneo la Micheweni ndio lililochaguliwa kuwa eneo maalum la milleniam. Ndio maana Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ikaamua kujenga Radio ya Jamii ili iwe ndio kichocheo cha kuharakisha maendeleo yaliyokusudiwa katika vijiji vya millenia ulimwenguni. Kwa hapa kwetu ni kijiji cha millenia cha Micheweni.

Naomba pia Mhe. Spika, kueleza kwamba radio hii mbali ya kuwa kichocheo pia itaharakisha maendeleo ya wananchi wa Micheweni kwa kuyafanya mawasiliano ya habari kuwa katika milki yao. Ndio maana kutakuwa na chumba maalum cha TEKNOHAMA, yaani Teknolojia ya Habari na Mawasiliano mahususi iliyokusudiwa kwa wana jamii wa hapo Micheweni.

Kwa kawaida Radio zote za jamii Mhe. Spika, ulimwenguni huwa ni mali ya jamii yenyewe ambayo huendeshwa na wanajamii wenyewe.

Kwa kutoa msukumo huo serikali kwa kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeamua kuajiri vijana kutoka Micheweni, kuweza kuisimamia Raido hii ili iweze kuzaa matunda yaliyokusudiwa. Hivi sasa tayari vijana hao wapo masomoni ili kupata taaluma ya kuendesha kituo hicho.

Mbali na Radio Jamii, kituo hichi pia kitatoa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na pia itakuwa ni mahali ambapo wana Micheweni wanaweza kupatumia kwa ajili ya kupanga shughuli zao za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni kwa kupata fursa hii adhimu.

Naomba sasa jimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina mpango kwa sasa kujenga majengo mengine ya Raido Jamii katika maeneo mengine ya kisiwa cha Unguja au Pemba kutokana na mazingira yake kuwa tofauti na Micheweni. Nia ya serikali ni kupima mafanikio yatakayojitokeza katika Radio ya Jamii Micheweni na baada ya hapo tutatizama mazingira mengine maalum katika nchi yetu yatayohitaji Raido Jamii kama hiyo. Aidha, wenzetu washirika wa maendeleo na hasa *UNESCO* pamoja na *UNDP* wameonyesha nia yao ya kutaka kutusaidia kufanikiwa katika lengo letu hili.

(b) Jengo hilo la Micheweni mpaka kumalizika kwake Mhe. Spika, litagharimu jumla ya Tshs.157,400,000/= kwa ujenzi wa Jengo lenyewe, na Tshs. 45,000,000/= kuweka "*Transformer*" na kuvuta umeme wa "*high-tension*" hadi kufikia katika kituohicho.

Gharama hizi za jengo, umeme pamoja na ujenzi wenyewe zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Naomba nichukue fursa hii kujipongeza sisi wenyewe serikali kwa kuweza kupata fedha hizi na zote kukamilika kwa wakati, ambapo sasa hivi ujenzi umepita ule muda uliopangwa hadi kupata sifa maalum kutoka *UNESCO*. Vifaa vya radio hiyo pamoja na gharama za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano vinakadiriwa kugharimu Tshs.100,000,000/= ambazo zitagharamiwa na Shirika la Elimu Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa, yaani *UNESCO*.

(c) Ni kweli kuna mpango wa kujengwa nyumba mbili za wafanyakazi wakati wowote mwishoni mwa mwaka huu na mwanzoni mwa mwaka ujao 2010, pale tutakapokamilisha kituo kikiwa kimeshaanza kufanyakazi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza naipongeza serikali kwa hatua iliyofika ya kuwajengea Radio Jamii Micheweni.

Mhe. Spika, mimi kama mjumbe wa kamati, nathibitisha kwamba hatua iliyofikiwa ni nzuri na jengo linapendeza sana. Hivi sasa wako katika hatua za mwisho za kutaka kuweka vifaa.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisema kwamba Radio Jamii Micheweni imejengwa kwa mazingira yake ya Kimicheweni na akasema Mhe. Naibu Waziri kwamba hawana mpango wa kujenga katika maeneo mengine

radio jamii, mpaka yaonekane kama yako maeneo ambayo yanafanana na Micheweni.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri, kule Kijini Wilaya ya Kaskazini A Mkoa wa Kaskazini katika Jimbo la Matemwe, Je, haifanani na Micheweni na kama inafanana kimaendeleo na kimazingira ana mpango gani wa kuwasaidia watu wa kijini kujenga Radio Jamii?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba kueleza kwamba katika mpango wa vijiji vya millenia, mpango ambao umepangwa na Umoja wa Mataifa na nchi mbali mbali kusaini, huwa wanaangalia mambo matatu muhimu ili uweze kuingia katika mpango huo.

1. Idadi ya watu, yaani *population.*
2. Masafa kufikia kwenye zile huduma muhimu za kijamii,
3. Uchumi wa ile sehemu yaani hali ya umaskini na uchumi wa watu katika eneo lile.

Sasa nasikitika kusema kwamba Jimbo la Matemwe halitoweza kuingia katika mpango huu, kwa sababu ya uchumi wake eneo hilo la Matemwe ni mzuri na zile njia kuu za kupata vipato ni mzuri zaidi kuliko eneo la Micheweni. Kwa hivyo, hapo haitoweza kuingia Radio ya Jamii, ila kwa ule mpango mwingine niliyosema hapo awali kwamba tunaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo, kama kutaonekana ipo haja na Mheshimiwa na yeye awe karibu na sisi katika kuzungumza suala hilo ili tuweze kushirikiana kuzungumza na washirika wa kimataifa. Ikionekana ipo haja ya kupata Radio Jamii huko, basi hapo baadaye tutakapoweza kufanikisha tutaweza kumsaidia katika hilo.

Nam. 49

Muuguzi Mwenye Matatizo ya Uti wa Mgongo

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kupitia Bodi yake ya Wakurugenzi ndio inayotoa idhini ya mgonjwa kwa kusafirishwa nje kwa matibabu baada ya Daktari Mtaalamu wa maradhi kukubali kuwa tatizo la mgonjwa huyo haliwezi kutatuliwa hapa petu. Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili na hapo ndio hutolewa kibali cha kupelekwa nje kwa matibabu na Daktari hufanya makisio ya matibabu ya mgonjwa na Daktari anaekwenda nae.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kuwa katika Kituo cha Afya Mtambile pana muuguzi mwenye matatizo ya uti wa mgongo na kusababisha kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa kwa kusimama tu ?

(b) Kama unalifahamu tatizo hilo Je, Wizara imetoa msaada gani wa matibabu kwa muuguzi huyo ?

(c) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa muuguzi huyo kutoa huduma kwa kusimama kutwa hawezi kukaa kwa matatizo yake ni usumbufu ?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vifungu (a),(b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu ya Afya na Ustawi wa Jamii inajua kuwa katika kituo cha Afya Mtambile pana muuguzi mwenye matatizo ya Uti wa Mgongo.

Mhe. Spika, ili kutatua matatizo hayo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekuwa ikimpatia matibabu katika kitengo cha matibabu ya viungo, pamoja na dawa za kupunguza maumivu. Sambamba na hayo mgonjwa huyo tayari imeshafanyiwa uchunguzi na Bodi kwa lengo la kumpatia rufaa ya matibabu zaidi nje ya nchi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa bahati taarifa hii ilikuwa tuitoe kwenye taarifa, lakini madhali imeulizwa swali, basi tunaweza kuliongezea hapa hapa akapata faida yeye Mhe. Waziri pamoja na Baraza lako tukufu na yeye mwenyewe anatusikiliza huko aliko.

Mhe. Spika, muuguzi huyu ana malalamiko ya muda mrefu na kutokana na hali yake aliyokuwa nayo Mheshimiwa, tunaamini ni mfanyakazi mzuri na mwenye uzalendo wa nchi yake. Kwa sababu pamoja na kusumbuliwa na maradhi hayo, lakini anasema mimi sijawa tayari kulala nyumbani niko tayari kufanyakazi kwa masaa yaliyokubalika. Kwa kuwa tunamtumia na yeye anatumikia wananchi.

Je, Mhe. Waziri haoni kuna umuhimu wa haraka wa kumpatia huduma ambayo inahitajika ya matibabu mazuri ili mwenzetu huyu aishi vizuri, hasa tukizingatia kwamba kila akikaa na maradhi yanazidi.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa haraka wa kumuharakisha mtu huyu ili kumpeleka matibabuni ili apate unafuu wa haraka.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kama nilivyokwisha mjibu kwamba mfanyakazi wetu huyu tayari bodi imeshamuona na yumo katika matayarisho ya kuangalia uwezekano wa kumpeleka nje ya nchi kwa matibabu zaidi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza namkubalia Mhe. Waziri kwamba bodi imeshakaa na imefanya makisio. Kwa kuwa bodi imekaa na imefanya makisio, bila shaka utaratibu umeshakamilika. Naomba nimuulize Mhe. Waziri.

(a) Kama kweli wameshafanya makisio je, mgonjwa huyu atasafirishwa kwenda nchi gani?

(b) Ni kiasi gani gharama yake imepangwa?

(c) Ni nini tatizo ni wizara yake au Wizara ya Fedha, utaratibu upo kwa nini wamnyime nafasi au wamnyime fedha mgonjwa huyu kwenda nje?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kiutaratibu itabidi mgonjwa aangaliwe na bodi na ikishamwangalia madaktari watatu wale wanaleta maoni yao kwa mkurugenzi mkuu au katibu mkuu. Baadaye wanawasiliana na hospitali husika kwa kuletewa makisio ya matibabu hayo, ndipo inapokuja kwenye meza yangu na mimi huomba fedha katika Wizara ya Fedha kwa ajili ya kusafirishwa mgonjwa huyu. Bado bodi haijaleta mambo hayo kwenye meza ya Mkurugenzi Mkuu au Katibu Mkuu. Tunachoambiwa Mhe. Spika, ni kwamba bodi imekwishamuona

Mhe. Spika, naomba kujibu hivi sipendi kudanganya Baraza lako tukufu, napenda kuweka wazi jibu la wazi kabisa. Ni kwamba bodi imekwishamuona baadaye bodi hiyo au madaktari hao watatu wataleta kwenye meza ya Katibu Mkuu au Mkurugenzi Mkuu, watawasiliana na hospitali husika. Hospitali husika itasema matibabu haya ni kiasi kadhaa. Baadaye mimi baada ya kupewa makisio yale ndipo ninapoomba Wizara ya Fedha inipatie gharama ya fedha zile kumruhusu mgonjwa yule kwenda kutibiwa nje ya nchi. Sasa tupo kwenye sehemu ya bodi na tunasubiri tupate makisio yake kutoka nje ya nchi ndipo nimuombee fedha hizo. Mhe. Spika, nafikiri nimefahamika *(Makofi)*.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri anaweza kutueleza ni kwa muda gani maalum anaohitajika mgonjwa aliyekwisha kukaliwa na bodi kupelekwa matibabu nje ya nje? Kwa sababu tayari kuna wagonjwa ambao wameshakaa zaidi ya mwaka mmoja, yaani bodi ilikaa na bado hawajapelekwa matibabuni.

Je, ni muda gani maalum ambao Wizara imejipangia kwamba mgonjwa baada ya bodi kukaa na kupitisha anaweza kupelekwa matibabuni nje ya nchi?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza lazima afahamu Mhe. Mwakilishi hivi karibuni alikuwepo *Myott* na wagonjwa wetu kutoka Zanzibar wapo *Myott*. Kwa makubaliano ya Hospitali ya *India Myott* kwamba wagonjwa wakesha kutibiwa zinaletwa gharama Zanzibar na Wizara ya Fedha na Uchumi inalipa gharama hizo, zikeshakulipwa ndio tunapaswa tupeleke wagonjwa wengine. Kwa hivyo, tunapeleka, tunalipa, tunapeleka na kulipa na huo ndio utaratibu uliopo Mhe. Spika *(Makofi)*.

Kwa kweli juu ya meza yangu Mhe. Spika, kuna maombi yasiyopungua 40 kwa ajili ya kupelekwa nje ya nchi ya Zanzibar kwa matibabu hata bajeti ya Wizara ya Afya haikidhi haja hiyo.

Nam. 32

Usajili wa Simu za *ZANTEL*

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Hivi sasa Kampuni ya Simu ya *ZANTEL* hapa petu imeanza kazi ya usajili simu zake kwa kujaza fomu maalum, pia inawekwa na picha moja ya *Passport size*. Vile vile *copy* ya kitambulisho cha Mzanzibar huna *copy* ya *Passport* na kama huna basi *copy* ya kitambulisho cha kazi na zoezi hili litamalizika katika mwezi wa Disemba 2009. Zoezi hilo kwa sasa ni bure hutoi gharama yeyote ile isipokuwa muda huo uliowekwa ukimalizika patakuwa na gharama yaani faini.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili una lifahamu?

(b) Je, Mhe. Waziri zoezi hili lina faida gani kwa wateja na kwa kampuni ili wananchi wajuwe?

(c) Je, Mhe. Waziri wale waliochelewa muda wa bure wa usajili faini itakua kiasi gain?

(d) Je, Kampuni nyingine za simu kama *CELTEL*, *TIGO*, *TTCL* na kadhalika wao hawana zoezi kama hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza, ili kutekeleza majukumu wetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vifungu (a), (b), (c), na (d) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kuwa ni kweli Kampuni ya *ZANTEL* pamoja na Kampuni zote za Simu nchini ikiwemo *VODACOM*, *CELTEL*, *TIGO* na *TTCL* zimeaza kazi ya usajili wa simu kwa kujaza fomu maalum, ambapo mteja hutakiwa kuweka picha ya *passport size*, *card number* ya simu, kopi ya kitambulisho chochote ambacho mteja anacho.

Utaratibu huu umeweka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ambapo imezitaka kampuni zote nchini kuanza utaratibu wa kuandikisha *sim card* zote za simu nchini. Hivyo kampuni zote zimetakiwa kuruhusu namba zote ziliopo kwenye mtandao yao kutambulika kwa mpokeaji wa simu.

Madhumuni ya hatua hii ni kuhakikisha kuwa wamiliki wote na namba za simu wanaandikishwa, ili kujulikana kila mmoja na simu yake. Baadaye kufuatilia utumiaji wa simu, ili kuona kama kutatokea matumizi mabaya ya simu na namba za simu hizo za *card* basi hatua za kinidham zichukuliwe.

Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, unapokwenda kujisajili kwenye Kampuni ya *ZANTEL* wanahitaji picha pamoja na *copy* ya kitambulisho, lakini mitandao mingine kama vile *ZAIN*, *VODACOM* wao hawataki picha isipokuwa ni kitambulisho tu. Kwa hivyo, jambo gani lililopelekea Kampuni ya *ZANTEL* kutaka picha na hao wengine wasihitaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba hizi ni kampuni tofauti, kwa hiyo kila mmoja inakuwa na utaratibu wake ambao imejiwekea.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Kampuni ya *ZANTEL* inasajili simu, ili kuondoa vurugu na zaidi kinachoangaliwa mule ni *sim card*, lakini bado *sim card* zinauzwa madukani. Je, hivi hizi *sim card* ziliomo madukani watadhibiti vipi, kwa lengo lile la kuondoa vurugu kwenye simu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Mwakilishi labda pengine bado hajasajili simu yake na ndio maana hajaelewa utaratibu mzima uliopo. Kwa sababu kinachotakiwa pale sio *sim card* tu, isipokuwa pia kuna *serial number* ambayo imo ndani ya simu na wala haibadiliki. Kwa hivyo, mtu anapopiga simu kwa mfano Mhe. Ame Mati Wadi amepiga simu na kumtukana mtu *(Makofi)*.

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea kuna matangazo mawili. Kwanza kuna tangazo ambalo linalingana na swali tulilolimaliza hivi sasa, kwamba ndugu zetu wa Kampuni ya *ZANTEL* wameongeza muda na leo wamekuja, kwa ajili ya usajili wa simu zetu na sijui leo watakaa wapi, kwa sababu ukumbi wa juu kuna kamati inataka kwenda kukaa. Sasa mtapewa taarifa wako wapi, lakini wapo katika afisi yetu.

Pili Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, itakaa kwenye ukumbi wa juu, kwa ajili ya kumaliza shughuli ya mswada unaohusina na madawa ya kulevya. Kwa hivyo, mara nitakapokaa kitako wakati wajumbe wote pamoja na Mwenyekiti yupo pale ambaye yupo tayari, basi mtaongozana kwa ajili ya kwenda kumaliza kazi hiyo, ili kesho semina yetu iende vizuri juu ya mswada huo.

Baada ya matangazo hayo sasa tuendelee.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 mwaka 1996

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru sana kunipatia fursa hii kwa ajili ya kuwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 mwaka 1996.

Mhe. Spika, tumejitahidi kutoa *photocopies* ya sheria yenyewe kama ilivyo. Kwa hivyo, ningeomba sana Waheshimiwa sote tuipate *copy* kwa urahisi wa

kufanya yale au kufuatilia marekebisho. Kwa sababu si marekebisho makubwa, lakini ni muhimu sana ndio maana tumeona tutoe *photocopies* sheria yenyewe, ili sote tuweze kufanya rejea kwa urahisi sana.

Mhe. Spika, kama Baraza lako tukufu linavyofahamu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua hatua kadhaa, zinazolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato nchini, hususan kwa mapato ya ndani yanayosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar, yaani *Zanzibar Revenue Board*.

Hatua hizi zimehusu maeneo ya mfumo wa sheria, ujenzi wa bodi yenyewe kama taasisi, mafunzo na ujuzi kwa watendaji, vile vile kuipatia bodi vifaa vya kisasa pamoja na nyenzo za kufanyiakazi.

Mhe. Spika, kuhusu mfumo wa sheria Serikali imekuwa ikifanya mapitio ya mara kwa mara sheria za kodi, ili kuhakikisha kwamba hazipitwi na wakati na zinasaidia sana katika usimamizi bora wa mapato.

Naomba kuweka kwenye kumbukumbu shukurani za Serikali kwa Baraza lako tukufu kwa mchango mkubwa wa ushauri, maelekezo na hata pongezi kwa Serikali kuhusiana na utendaji wa Bodi yetu ya mapato. Mhe. Spika, tunakumbuka bodi ilivyoanza makusanyo yake kunako labda bilioni 1 na leo tunafika bilioni 7 kwa mwezi. Kwa kweli ni ya kupigiwa mfano na bado mapendekezo au ushauri mnaotupa hapa Barazani tunaupokea na kuufanyiakazi kwa kuleta ufanisi katika chombo chetu hiki kikubwa cha kukusanya mapato.

Mhe. Spika, mswada unaowasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu ni muendelezo wa hayo marekebisho au Serikali kufanya marekebisho ya sheria zinazohusu *ZRB*, ili kuweza kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato. Tutakumbuka kwamba jana katika Baraza hili tukufu tulipitisha Mswada wa Sheria Mpya wa Kuweka Masharti ya Usimamizi wa Sheria ya Kodi na Mambo yanayosiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kutoa shukurani zetu za dhati kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Serikali kwa ujumla kwa Baraza lako kwa kuukubali na kuupitisha mswada huo.

Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) imeanzishwa rasmi chini ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 mwaka 1996 kama wakala pekee wa Serikali wa ukusanyaji wa kodi.

Wakati huo tulianzisha sheria zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato zilikuwa saba (7) na nilizitaja nilipokuwa nikiwasilisha mswada uliopita, lakini si vibaya kuzirejea tena kama hivi ifuatavyo:-

1. Sheria ya *Value and Tax Act* Nam. 4 mwaka 1989
2. Sheria ya *Stamp Duty* Nam. 6 mwaka 1996
3. Sheria ya *Hotel Levy* Nam. 1 mwaka 1995
4. Sheria ya *Port Service Charge* Nam. 2 mwaka 1999
5. Sheria ya *Petroleum Levy* Nam. 7 mwaka 2001
6. Sheria ya *Property Tax* Nam. 14 mwaka 2008 na
7. *The Trade License Act* Nam. 3 mwaka 1983.

Kwa hivyo, tutakuta Bodi yetu ya *ZRB* imejikita kwenye sheria ndogo hizi au inafanyakazi zake kwa kuongozwa na sheria hizi saba (7) nilizozitaja, ambazo jana tulizifanyia marekebisho yake, ili mtiririko wake uwe mmoja.

Mhe. Spika, madhumuni na sababu ya mswada huu ninauwasilisha leo yameelezwa kwa ufupi kwenye ukurasa wa 53 wa mswada. Wakati lengo kuu la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa bodi (*ZRB*).

Naomba nieleze kwamba madhumuni ya mswada kwanza kuondoa utata katika kutumua hili neno la bodi, baina ya bodi kwa ujumla wake kama taasisi, yaani *Zanzibar Revenue Board* na Bodi ya Wakurugenzi ya *ZRB* kama ilivyotumika katika sheria hiyo.

Mhe. Spika, ni muhimu sana kuondoa utata huu kwani nako kunapelekea uwekaji bayana wa majukumu baina ya bodi ya Wakurugenzi na uongozi, yaani *management*. Sheria ya sasa inataja bodi bila ya kubagua iwapo majukumu husika ya ngazi ya wakurugenzi au *ZRB* kama taasisi na hivyo ya uongozi.

Matarajio yetu ni kwamba ufanisi utaimarika kwa kuweka wazi ngazi yenye jukumu la kusimamia kazi maalum zinazotajwa kwenye sheria na kuondoa uwezekano wa kutokea mgongano usio wa lazima. Vifungu vitakavyohusika na marekebisho haya vimetajwa kwenye ukurasa wa 50 wa mswada wenyewe.

Mhe. Spika, nadhani tukiuangalia ukurasa wa 50 unaonesha wazi pale marekebisho ya vifungu vya 5 na 6 vinaelezea kazi za bodi na kazi hizo zitakuwa zifuatazo kuanzia (a) mpaka (f). Kwa kweli hii imewekwa wazi makusudi tofauti katika sheria za zamani ambazo hazikuwekwa kwa uwazi.

Kwa upande mwengine mswada pia unakusudia kufanya marekebisho madogo katika muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ya *ZRB*, yaani *Board of Directors*. Lengo kuu ni kuleta uwiano baina ya muundo wa bodi na uhalisia wa muundo wa Serikali kuu. Miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi chini ya Sheria ya sasa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mipango.

Mhe. Spika, kama tunakumbuka sheria hii ilipitishwa wakati muundo wa Serikali kulikuwa na Wizara hiyo ya Mipango na Vitega Uchumi ambayo kwa sasa haipo tena. Kwa hivyo, mswada umeweka kifungu kitakachoruhusu kuingia kwa Katibu Mkuu atakayeshughulikia masuala ya fedha na yule atakayeshughulikia masuala ya uchumi, pindipo itatokea muundo wa sasa wa Wizara kubadilishwa kwa kutenganishwa masuala ya fedha na uchumi.

Muundo mpya wa Bodi ya Wakurugenzi unaonekana chini ya vifungu vya 5 na 6 vya mswada katika ukurasa wa 51 na 52.

Mhe. Spika, kazi na uwezo wa Bodi ya Wakurugenzi zimeainishwa chini ya vifungu vipya vya 8 (a), (b) na (c) kwenye ukurasa wa 52. Kwa hivyo, hizi ni tofauti na kazi za Bodi kama taasisi, yaani *ZRB* zilizowekwa chini ya kifungu cha 4 cha mswada kilichopo ukurasa wa 50.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wayapokee, wayajadili na hatimaye waidhinishe Mapendekezo haya ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 mwaka 1996, kwa madhumuni niliyoyaelezea.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena natoa shukurani zangu za dhati kwa kupata wasaa huu wa kunisikiliza.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mwanzo sikuona Mjumbe aliyesimama nikasema sasa basi mswada Mhe. Waziri aende nao mpaka baadae, lakini bahati nzuri hoja imeungwa mkono kwa maana hiyo mswada uko tayari kuweza kujadiliwa.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Ali Abdalla Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Mswada wa Sheria ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar ya Nam. 7 ya mwaka 1996 , leo tarehe 29 Oktoba, 2009.

Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha siku ya leo kuendelea kuwa hai na tukiwa wazima na afya njema. Tukiwa tumekusanyika tayari kufanya kazi tulizotumwa na wananchi wetu.

Pili nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa uwasilishaji wake mzuri. Shukurani hizi ziwaendee pia Makaimu Waziri wake ambao walikuwa wakiyatimiza majukumu wakati alipokuwa hayupo kwa dharura maalum.

Aidha, niwapongeze watendaji wakuu na wadogo wa Wizara hii ya Fedha na Uchumi wakiongozwa na Katibu Mkuu na Manaibu wake. Na kwa mswada huu pongezi hizi ziwaendee hasa Kamishna na Naibu wake pamoja na Watendaji wake wote wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa juhudi zao za kukusanya na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya nchi kwa niaba ya Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kupongeza na kuwashukuru wajumbe wenzangu niliokuwanao kwenye kamati yetu ya Fedha na Uchumi kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa, Wajumbe wenyewe ni:-

1)	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2)	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	M/Mwenyekiti
3)	Mhe. Assaa Othman Said	-	Mjumbe
4)	Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	-	Mjumbe
5)	Mhe. Ashura Abeid Faraji	-	Mjumbe
6)	Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	-	Mjumbe
7)	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
8)	Mhe. Said Khelef Ali	-	Mjumbe
9)	Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	Mjumbe
10)	Nd. Amour Moh'd Amour	-	Katibu

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar ndio wakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zamzibar katika suala zima la ukusanyaji wa mapato. Huu ni utaratibu unaotumika duniani kote, kwamba ili Serikali zijiendeshe na zijenge mustakbali mzuri wa maisha ya watu wake, ni lazima zikusanye kodi.

Mhe. Spika, ili uwakala huu uwe madhubuti, ni vyema muundo wa Bodi nao uendane na mazingira ya wakati uliyopo kwa kadiri mazingira hayo yatakapobadilika basi miundo nayo ibadilike. Hivyo mapendekezo na marekebisho ya sheria au kanuni nayo yawe na mtazamo wa kujenga uwezo wa Bodi na kuiwezesha kufanya kazi zake vyema na ukamilifu.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kazi ambayo tumeipa taasisi hii ya kusimamia na kukusanya kodi ni kubwa, inahitaji ujasiri, uadilifu lakini pia na mipango endelevu yenye kuimarisha mbinu bora na wepesi wa upatikanaji huo wa mapato. Miundo mbinu ambayo inamuezesha mkusanyaji kupata urahisi wa

kazi yake na mlipa kodi nae hasumbuliwi katika kutimiza wajibu wake huo wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, haya ndiyo yanayopelekea kutungwa sheria na kanuni mbali mbali zenye kuonesha njia ya kufikia hayo malengo ya ufanisi ili iuweze kuinua uchumi wetu na hali za wananchi wetu ambao ni wanyonge.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria uliopo mbele yetu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996 kwa madhumuni ya kuleta utekelezaji mzuri wa sheria hiyo na hivyo kuongeza ufanisi katika kutekeleza jukumu kubwa na umuhimu wa Bodi ya Mapato Zanzibar kufikia malengo.

Mhe. Spika, katika marekebisho haya yanayokusudiwa kufanywa, kuna baadhi ya vifungu vya sheria mama (Sheria Nam. 7 ya 1996) vinafutwa na kuwekewa vifungu vipya, lakini pia kwa kutoa tafsiri nyengine ya maneno ili iendane na mabadiliko hayo ya vifungu hivyo. Kwa mfano, vifungu vya 5 na 6 vinafutwa ambapo sasa vinawekwa vizuri kazi za bodi kwenye kifungu cha 5 na kwenye kifungu cha 6 kinaeleza uwezo wa Bodi.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba mambo yanaenda vizuri na bila ya kuwa na mgongano wa majukumu, marekebisho haya yanakusudia kuanzisha bodi mpya ambayo itajulikana kama Bodi ya Wakurugenzi. Muundo, kazi na uwezo wa bodi hiyo ya Wakurugenzi unaelezwa kwa kufuta kifungu cha 8 cha Sheria Mama kwa kuweka vifungu vya 8A, 8B na 8C mara baada kifungu kipya cha 8.

Mhe. Spika, kamati yangu haina pingamizi hata kidogo juu ya marekebisho haya, inachosisitiza zaidi ni ushirikishwaji wa sekta binafsi ambazo kwa kweli hao ndio wadau wakubwa, na ndio maana katika marekebisho hayo kwenye kifungu cha 8 (2) (f) imependekeza kwenye suala la uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi inayoundwa basi kwenye wajumbe watatu watakaoteuliwa na Waziri, basi angalau mmoja atoke kwenye sekta au taasisi binafsi.
Mhe. Spika, tunasisitiza sana haya mahusiano na sekta binafsi kwani ni wadau wanaohusika watakapohisi kwamba maamuzi ya utekelezaji wa sheria au kanuni yamewasilishwa na wao, basi huwa ni rahisi katika kuifikisha elimu kwa walengwa wa chini kabisa, lakini pia utekelezaji unakuwa rahisi na wa hiari; na huko ndiko kutakuwa na mafanikio mazuri.

Mhe. Spika, kazi na uwezo unaokusudiwa kupewa kwa Bodi ya Wakurugenzi unatoa mwelekeo mzuri wa mafanikio endapo tu utekelezaji wake utakuwa kama ulivyokusudiwa. Kamati inaweka matumaini makubwa kwamba, ipitapo

sheria hii basi bodi hiyo itafanya kazi zake bila ya woga wala chuki na kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na Kamati yangu ya Fedha na Uchumi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono hoja hii pamoja na marekebisho yake, basi naomba pia Waheshimiwa Wajumbe na wenzangu wote tuuchangie mswada huu na hatimaye kuunga mkono Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny: Mhe. Said Ali Mbarouk – Waziri Kivuli Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema siku ya leo na kuweza kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi na taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, pia napenda kwa nafasi ya kipekee kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya kambi ya upinzani. Mhe. Spika, mswada huu unazingatia kufanya mabadiliko ya jumla ya vifungu vinne (kifungu 2, 5, 6 na 8) vilivyomo ndani ya ya Sheria ya Bodi ya Mapato Nam. 7 ya mwaka 1999 kwa madhumuni ya kuleta ufanisi mzuri katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, kabla ya kuingia katika maudhui ya mswada wa sheria hii, masuala ya msingi ambayo kambi ya upinzani inataka ipatiwe majibu ya kina na ya ufasaha ni kama yafuatayo:-

> Je, Bodi ya Mapato kama chombo cha ukusanyaji wa kodi imesimama vizuri katika sheria yake?

Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli nzima ya utayarishaji na upitishwaji wa miswada ni shughuli inayochukua muda wa wataalamu, wanasheria, wadau mbali mbali na hatimaye Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ni wazi si muda tu unaotumika bali pia shughuli hii ina gharama kubwa kutokana na vikao mbali mbali hadi kufanikisha.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaishauri Serikali inapoleta hasa inayohusiana na mabadiliko ya sheria zilizopo basi ni bora ikawa makini kuzipitia sheria hizo kwa kina ili kufanya mabadiliko ya pamoja badala ya kuwa na mabadiliko ya mara kwa mara.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo serikali itaweza kuokoa muda na gharama inayosababishwa na sheria moja kufanyiwa mabadiliko mara kwa mara. Je, hakuna mapungufu zaidi ya haya marekebisho ambayo yamewasilishwa ndani ya mswada huu tunaojadili ambayo nayo yangepaswa kuletwa pamoja na mabadiliko haya.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo kambi ya upinzani inataka ipatiwe majibu ni kuhusu ushirikishwaji wa wadau. Mhe. Spika, dhana ya kuwashirikisha wadau katika utayarishaji wa sheria ambazo zinawahusu imeshika kasi zaidi katika miaka ya hivi karibuni, kwa kuwa Sheria ya Bodi ya Mapato ina miaka zaidi ya 10. Kambi ya upinzani inataka kujua je, wadau wameshirikishwa vipi katika kuzipitia sheria za kuwepo Sheria ya Bodi ya Mapato.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala la kulipa kodi ni wajibu na haupaswi kutegemea ari ya mlipa kodi katika kifungu cha 4 cha mswada huu wa sheria kambi ya upinzani inashauri kuwekwa neno uwajibikaji baada ya neno ari. Hivyo, kifungu cha 4© kisomeke "kuongeza uwajibikaji wa kulipa kodi kwa hiari na kuongeza ukusanyaji wa mapato".

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6(d) na mswada huu wa sheria kambi ya upinzani inataka kufafanuliwa kwa maana ya maneno yafuatayo. Waziri kwa maandishi ya mkono wake. Mhe. Spika, hapa inakusudia nini? Je, ikiwa waziri atachapisha maelekezo hayo na baadae akaweka sahihi yake itakuwaje?

Mhe. Spika, katika kifungu hicho hicho kwa kuwa maelekezo hayo hayakuwekewa mipaka, kambi ya upinzani inataka kueleweshwa. Je, ikiwa waziri atatoa maelekezo hayo na yakawa yako kinyume na taratibu za utendaji wa bodi au kinyume na maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi, maelekezo hayo yatachukuliwa vipi?

Mhe. Spika, iwapo waziri atatoa maelekezo hayo kwa madhumuni ya kujijengea maslahi yake binafsi au ya jamaa yake je, bodi itawajibika kutekeleza maelekezo hayo. Mhe. Spika, katika kifungu cha 8(2) cha mswada huu wa sheria katika kifungu kidogo cha (f) kwa kuzingatia umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo yetu, kambi ya upinzani inashauri katika nafasi hizo tatu basi angalau mbili ziwe za wanaotoka sekta binafsi.

Mhe. Spika, katika hili tunashauri mfano mzuri ulioneshwa na serikali wa kutenga nafasi mbili kati ya nafasi nne ambazo Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji atateua katika Bodi ya Wakurugenzi ya Kamishna ya Utalii nafasi mbili kutoka sekta binafsi.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani kwa hivyo inashauri kifungu 8(2f) kisomeke kama ifuatavyo:

"Si zaidi ya wajumbe wengine watatu watakaoteuliwa na waziri wenye taaluma na uzoefu katika mambo ya fedha, biashara, uchumi, kodi au sheria ambao hawana maslahi binafsi katika bodi na angalau wawili kati yao watokane na sekta binafsi zinazohusiana na fani zilizoanishwa hapa".

Mhe. Spika, Bodi ya Wakurugenzi ni chombo kinachotarajiwa kuisimamia Bodi ya Mapato katika kifungu cha 8 kifungu kidogo cha (2c) Kamishna wa Bodi ya Mapato nae anaingizwa kuwa ni mjumbe katika Bodi hiyo ya Wakurugenzi. Mhe. Spika, kambi ya upinzani inashauri Kamishna asiingizwe kama Mjumbe wa Bodi na badala yake aweze kuingizwa katika *secretariat.*

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaona mabadiliko hayo ni muhimu sana, hasa kwa kuzingatia kifungu cha 8C(1) (a) na (b) vinavyozungumzia juu ya uwezo wa bodi naomba kuvinukuu vifungu hivyo vinavyoelezea juu ya uwezo wa bodi;

Kifungu cha 8C(a) na (b)

> "Kumtaka Kamishna kutoa taarifa yoyote, ripoti au nyaraka zozote ambazo bodi inaona muhimu kwa utekelezaji wa kazi kazi zake"
>
> "Kutoa maagizo ya kisheria kwa Kamishna kuhusu uendeshaji na utendaji wa bodi".

Mhe. Spika, hapo kambi ya upinzani inashangazwa kuona wakati huo huo mtu ambaye anataka kusimamiwa na Bodi ya Warugenzi nae anakuwa ni mjumbe ndani ya bodi hiyo hiyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 8A(2) naomba kukinukuu.

> "Mwenyekiti ataitumikia ofisi kwa masharti na taratibu kama zitakavyoanishwa katika hati yake ya uteuzi kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu kwa muhula wa kwanza na anaweza kuteuliwa tena"

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaamini katika dhana nzima ya kutowaweka wahasibu, wakaguzi wa hesabu na hata viongozi waliopo kwenye nyadhifa zinazohusiana na mambo ya fedha kwa muda mrefu ili kuepusha suala la kuweza kuzoea mazingira hayo ambayo wakati mwengine huwa ni nyanzo cha ufisadi ndani ya vyombo vyetu. Mhe. Spika, tumezoea kuona watumishi wa

aina hiyo kupewa uhamisho mara kwa mara ili kuepusha matatizo yatakayoweza kutokea kutokana na kuzoea mno sehemu moja.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaamini nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ni nyeti na ina uhusiano moja kwa moja na masuala ya kifedha. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar ina Wazanzibari wenye uwezo wa kuweza kuteuliwa kushika wadhifa kama huo ni vyema basi uteuzi huo ukawa kwa kipindi kimoja tu ili kuwapa fursa Wazanzibari wengine nao kutumikia nchi yao.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inashauri pia kwamba Rais anapoteua iwe ni Wenyeviti wa Bodi au Wajumbe wa Tume mbali mbali basi ni vyema suala la uwezo wa kuajibika kwa wateuliwa hao ukazingatiwa. Mhe. Spika, kambi ya upinzani inapata mashaka makubwa kwa kuona mtu mmoja achaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi zaidi ya mbili na pia anakuwa Mjumbe wa Tume yenye majukumu makubwa. Je, ni kwa uwezo gani mkubwa au sifa za ziada anazokuwa nazo mtu wa aina hiyo ambao umekosekana kwa Wazanzibari wengine?

Mhe. Spika, kambi ya upinzani huwa inajiuliza je, uwajibikaji wa mtu wa aina hiyo unakuwaje. Mhe. Spika, ikiwa hakuna budi basi uteuzi huo uwe kwa kipindi kingine kimoja tu na si zaidi ya hapo. Mhe. Spika, kambi ya upinzani inashauri kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo:

> "Anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja chengine na si zaidi ya hapo".

Mhe. Spika, katika kifungu cha 8A kifungu kidogo cha (3) kifungu hiki kinampa Rais uwezo wa ziada, inawezekana uwezo huo ukatumika vibaya kwa kumuondoa Mwenyekiti ambaye hakubaliani nae kimawazo. Mhe. Spika, kambi ya upinzani inashauri kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na Bodi ya Wakurugenzi iwe ndio na uwezo wa kupigia kura ya kutokuwa na imani iwapo Mwenyekiti huyo atashindwa kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo nakushukuru na nawashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza. Mhe. Spika, kwa heshima zote naomba kuwasilisha.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante Mhe. Spika, kuweza kupata fursa hii na mimi kuweza kuchangia mswada ulioko mbele yetu. Kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Waziri kwa dhati kabisa na watendaji wake kuona kwamba kuna haja ya marekebisho ya Bodi ya Mapato ili kuweka yale ambayo yanahitajika katika utekelezaji wa kazi hizi.

Mhe. Spika, pia niwapongeze Kamati ya Fedha na Uchumi kwa yale ambayo wameyaona kama kuna marekebisho ya hapa na pale na wameweza kurekebisha na kuyaweka katika vile vifungu ambavyo vina kasoro.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana katika mswada huu kwa sababu kilichoandikwa hapa chote kimepitia katika sehemu za wataalamu na leo kiko hapa mbele yetu. Mimi ninachotaka kusema kwamba katika marekebisho ya kuanzishwa na kuundwa kwa bodi, bodi tayari imeundwa lakini ikawa na kasoro ambapo wale watendaji wenyewe watakapokuwa hawako tayari kufanya kazi hii. Hiyo nayo itakuwa ni kasoro si vyema kama mtu anapewa majukumu halafu baadae zile kazi ambazo ametakiwa kuzifanya akawa anazikwepa. Kwanza nitilie mkazo kuwa hii bodi isimamie majukumu yake ambayo tayari itakuwa imeshapewa na iwe na uwezo ya kusimamia hayo majukumu hasa kwa upatikanaji wa hizo kodi zenyewe.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya hawa ambao wanafuatilia kodi, wanaweza wakafuatilia kodi kule ambako zinakohusika lakini hatimae ikafikia sehemu yale waliyokwendea wakayaacha wakaanza kufanya mengine. Kwa hivyo, itakuwa si vizuri itakuwa tunainyima serikali mapato yake na serikali itakuwa haina uwezo wa kufanya kazi kwa sababu mapato yake mengi yatakuwa hayaingizwi. Mimi nataka wawe makini katika kufanya hili kwa mfano kuna baadhi ya mahoteli yanashindwa kulipa kodi kutokana na usimamizi mzuri, na kuna mahoteli mengine yanadanganya katika ulipaji wa kodi hizi.

Mhe. Spika, mtu huwa anaanzisha hoteli baadae anasema kwamba mimi bado sijaanza kazi, lakini hoteli imekwisha na huku fedha zinaingia kwani wageni huwa wanaingia yeye ukimuuliza anasema hajaanza kazi. Mhe. Spika, mtu kama huyu ni kwa makusudi anakwepa kodi na maana nikasema wasimamizi hawa wawe macho kabisa. Mhe. Spika, jambo hili nalo liwe chini ya usimamizi wa bodi waangalie nini tunachokifanya.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 52 kama vifungu vilivyofanyiwa marekebisho mimi hapa sina wasi wasi, lakini ningesema kwamba Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi atateuliwa na Rais hili sijakuwa na mashaka sana lakini inatakiwa ateuliwa mtu aliyekuwa muadilifu katika hizi. Pia awe mtu mwenye mashirikiano na wenzake na asiitumie ofisi kama vile ni yake, hiyo iwe ofisi ya Bodi ya Wakurugenzi ifanye kazi za kama inavyotakiwa. Mhe. Spika, bila ya kuathiri vifungu ambavyo vimeshazungumzwa na hili nalo ionekane kama ifanye kazi kwa uadilifu kabisa katika walipa kodi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 8 uwezo wa Bodi ya Wakurugenzi, bila ya kuathiri vifungu ambavyo tayari vimeshazungumzwa katika mswada huu na hili nalo lionekane kwamba hiyo bodi ambayo tayari imepewa uwezo huo wa

kufanya kazi basi isisite na uwezo huo. Ifanye kazi kwa uadilifu kabisa na ndipo watakapogundua yale mapungufu ambayo yanatokezea kwa walipa kodi.

Mhe. Spika, la mwisho kuna neno hapa Kanuni za Utumishi nafikiri bodi itakuwa na kanuni zake. Kwa hivyo, kimsingi ukianzisha kanuni inatakiwa yafuatilie kwa kina kanuni inavyotaka inawabana wale ambao wanahusika na kutokulipa au kutokuajibika kufanya kazi za bodi. Kwa hivyo, hii kanuni isiende upande mmoja ibane kila upande ambapo tayari itaweza kufanya kazi zake kwa uzuri kabisa.

Mhe. Spika, kwa kuwa nilisema sina mengi juu ya mswada huu kwani ulifanyiwa baadhi ya marekebisho tu. Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Nungwi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza na kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, pia nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii kuzungumza machache katika mswada huu ambao umeletwa mbele yetu unaozungumzia sheria ya kodi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa mimi nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta mswada huu wa marekebisho haya pamoja na kwamba ni machache lakini ni muhimu kwa maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Chaani tunaukubali mswada huu na tunaunga mkono kwa asilimia mia. Jengine ambalo ningelizungumza katika mswada huu

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nataka nitoe tangazo kwamba si muda mkubwa kutoka sasa nadhani waziri atakuwa yuko tayari kuweza kufanya majumuisho. Kwa hivyo nilijaribu kuwatuma watumishi wetu hapa ndani kuwaita Waheshimiwa Wajumbe, lakini sasa kazi imekuwa ngumu maana wengine wanaingia na wengine wanatoka. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kama hakuna dharura ambayo ni muhimu sana basi tubaki ili tumalize hii kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Ahsante sana Mhe. Spika, kama nilivyosema nataka nianze na kifungu cha 3(1) kinachozungumzia suala zima la ufafanuzi. Katika ufafanuzi Mhe. Waziri amezungumzia suala zima la kumbukumbu za hesabu na akaeleza maana ya kumbukumbu. Mimi

nataka niungane na Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwamba kuna umuhimu wa kuwepo neno hili la uwekaji na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu.

Mhe. Spika, inaonekana kwamba katika wizara na taasisi zetu za serikali kumekuwa na mapungufu katika suala zima la utunzaji na uwekaji wa kumbukumbu katika mawizara yetu. Mhe. Spika, hii inajitokeza mara nyingi katika kamati zako zinapopita katika mawizara inabaini hayo na kwa kweli wakati mwengine kunatokea masuala mengi ambayo yanayoulizwa kuhusu utunzaji na uwekaji wa kumbukumbu. Kwa hivyo, kuwepo kwa kifungu hiki kunaonesha umuhimu wa kuweka kumbukumbu ni jambo muhimu.

Mhe. Spika, hili halitoshi kwamba limewekwa hapa lakini wizara ningeiomba kwa makusudi kabisa ikahakikisha kwamba inawafanyia usaili wafanyakazi wake pia kuwasomesha jinsi ya utunzaji na uwekaji mzuri wa kumbukumbu za hesabu katika maeneo hayo. Mhe. Spika kwa sababu tunapozungumzia makusanyo hasa yanayohusiana na mambo ya kodi maana yake ili ufanye biashara basi lazima uwe na hesabu, watu wanasema: "Mali bila daftari hughibu bila ya habari" maana yake kama huna hesabu maana yake ni kwamba unaweza ukashtukia unafanya kazi ambayo haina tija. Kwa hivyo, ili tuweze kuwa na kazi ambayo ina tija basi tuwe na wafanyakazi ambao wana taaluma ya kazi hizi zinazohusiana na mambo ya hesabu.

Mhe. Spika, jengine ambalo sambamba na hilo ni uwekaji mzuri wa kumbukumbu bado sio mzuri kwa maana ya kwamba muekaji wa kumbukumbu anaweza akawa hana kitabu kinamuonesha hasa kuwa hiki ni kitabu ambacho wamekiandaa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu zake zote ambazo za hesabu katika eneo lake. Hilo ni jambo muhimu katika maofisi ya serikali au katika eneo lolote lile. Kwa hivyo, ningeomba lishughulikiwe vizuri kwa sababu hizo sheria zipo naomba zitiliwe nguvu tu kuona kwamba kila kinachofanywa kiwe na kumbukumbu na kinawekwa vizuri.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza ni ukusanyaji mzuri wa hayo mapato wenyewe unategemea zaidi na lile jambo ambalo nimelitaja mapema la uwekaji wa kumbukumbu, kwa sababu itakapokuwa unakusanya fedha na katika ukusanyaji wako wa fedha baadhi ya risiti zinapatikana na risiti nyengine hazipatikani maana yake kile ambacho kilichokuwa hakipatikani pale kiweze kupatikana kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, vile vile katika mswada huu ni kuhusu jambo ambalo hata Mhe. Waziri Kivuli amelitaja kuhusu Mkurugenzi kuwa ni Mjumbe wa Bodi. Mhe. Spika, hili haliwezekani unapomuweka Mkurugenzi awe Mjumbe wa bodi maana yake ni kwamba bodi inapoburuza na yeye anaingia katika mkumbo ule,

pengine mtendaji huyo ni mzuri lakini tu kwa sababu umemuingiza katika mahala ambapo si pake basi tatizo litajitokeza hapo. Mhe. Spika, Wajumbe wa Bodi wakifanya vibaya na yeye anawajibika vibaya kwani na yeye ataingia katika yale makosa ambayo yamejitokeza. Lakini unapomfanya huyu mtendaji awe peke yake asiingie hapo aingie katika zile sehemu ambazo zinamuhusu moja kwa moja kutoka na taaluma zake, basi itasaidia pengine bodi kufanya mambo ambayo anajua wakifanya vibaya maana kuna watu watakuwa wanawatizama kile ambacho kinafanywa.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa kulizungumza katika mswada huu ni kuhusu suala zima la usajili. Mhe. Spika, tunapozungumza suala la usajili, usajili kila mmoja anajua maana yake ni nini hili ni jambo muhimu kwa sababu unaposajili ndio unapojua idadi ya kile ambacho unacho. Kwa hivyo, ni muhimu tukawa na usajili ambao utakuwa na uhakika wa kujua idadi ya wafanyabiashara wetu wote kwa ujumla tuliokuwa nao. Tukipata idadi ya wafanyabiashara maana yake unaweza kupata juu ya kile ambacho unakihitaji kutoka kwa wafanyabiashara hao kwani itakuwa tayari umeshaweka makisio ya hesabu na mapato yatakayopatikana kwa sababu yote yamewekwa vizuri.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu risiti ni vyema tukawa na utaratibu wa sehemu moja tu ambayo itakuwa inatoa risiti ambazo zinatumika kwa nchi nzima, iwe ni kwa serikali au wafanyabiashara wapate risiti kutoka katika taasisi ambayo itatoa hiyo risiti inayotambulika. Tumekuwa tukisema kila siku hapa kwamba utunzaji mbaya wa risiti huwa inatukosesha mapato. Kwa hivyo, ningeomba taasisi zinazotengeneza risiti basi wafanyabiashara wote wakawa wananunua risiti hizo kutoka katika taasisi ambayo imewekwa na serikali ambayo inahusiana na mambo ya mahesabu pamoja na makusanyo ya fedha. Mhe. Spika, hili litasaidia kwa serikali yenyewe vile vile itasaidia kwa wafanyabiashara binafsi kuweza kuwapata kujua kile wanachokiuza na kile ambacho wamekichukua.

Mhe. Spika, ingekuwa vyema kwa wale ambao watamaliza hizo risiti basi wakasimamisha mauzo badala ya kutumia risiti ambazo zilizokuwa hazitambuliki kisheria. Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi nilikuwa na mchango mdogo katika mswada huu, lakini niendelee kusema mimi mwenyewe naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu mdogo tu katika marekebisho ya mswada huu. Lakini mheshimiwa mimi nimesimama kwa hiari yangu hukunikamatia.

Mhe. Spika, mswada huu marekebisho yake ni madogo sana kifungu cha 2, 5, 6 na 8. Marekebisho haya yamekuja kwa sababu yakuwapa meno zaidi *ZRB* katika kukusanya mapato. Mhe. Spika, mchango wangu mimi utakuja katika kazi za bodi katika kifungu cha 4(a) (ii) inasema sheria nyengine yoyote inayohusika na ukusanyaji wa mapato ambayo bodi imepewa na wizara, idara au mamlaka yoyote ambayo inasimamia sheria hiyo.

Mhe. Spika, hivi karibuni nimesikia kwamba Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wamewapa bodi hii ukusanyaji wa kodi ya ardhi. Sasa hii ni kuwapa nguvu zaidi kwa sababu *ZRB* kwa kweli wamejiandaa vizuri katika kukusanya kodi. Sasa ningeliomba kodi ya *income tax* pamoja na kodi ya kukuza ujuzi basi nayo wangepewa *ZRB.* Hawa wana uwezo wa kukusanya vizuri zaidi na tukiwapa hizi ni imani yangu kwamba watazikusanya vizuri na pato la taifa litakua.

Kifungu chengine ambacho nilitaka Mhe. Waziri anipe ufafanuzi ni kifungu cha 6(2)(a) kutumia mali zote za bodi zinazohamishika na zisizohamishika kulingana na bodi ya wakurugenzi itakavyoona inafaa, ikijumuisha waombaji wa mikopo kwa kuweka rehani mali zao.

Sasa hili suala la rehani kidogo limenishughulisha, kwa sababu kabla ya mapinduzi tulikuwa na mambo ya rehani, lakini baada ya mapinduzi Marehemu Mzee Karume aliyaondoa. Sasa rehani hii mimi sijaifahamu imekusudiwa nini hapa, ningeliomba Mhe. Waziri akatupatia ufafanuzi tukajua wamekusudia rehani gani hapa.

Hapo hapo chini kifungu (c), kufanya jambo lolote linalohusiana na uwezo wake wowote, nalo hili naona kama *power* kubwa kwa sababu uwezo wake wote atakupiga na ngumi pia huyu. Sasa nafikiri angetupa maelekezo amekusudia nini. Kwa sababu lugha za kisheria Mhe. Spika, wakati mwengine zinakuwa tofauti na unavyoifikiria wewe, pengine wamekusudia kitu chengine na mimi nikafikiri vyengine. Sasa ningeliomba na hili tukapatiwa ufafanuzi au kama kuna lugha nyengine ya kuliweka sawa likawa vizuri zaidi basi ingetumika. Kwa sababu hii kwa ninavyoona mimi kama nguvu za ziada mtu anaweza akatumia kwa uwezo wake wote aliokuwanao. Hii ni hatari Mhe. Spika.

Kwa kuwa mswada wenyewe ni mfupi, marekebisho madogo na marekebisho yenyewe ni kuwapa nguvu tu *ZRB* waweze kukusanya vizuri basi Mhe. Spika, mimi naunga mkono.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mswada huu mfupi unaohusiana na marekebisho ya ukusanyaji wa kodi.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia mswada huu kwa wakati huu ambao tulikuwa kabisa tunautegemea. Kama ulivyo mswada wenyewe kwamba ni mfupi basi pia utegemee michango yetu nayo haitoweza kuwa mirefu.

Mhe. Spika, mimi kidogo tu nizungumzie suala zima la kumuweka Kamishna wa Bodi ya Mapato kwamba naye ni mjumbe wa suala hili. Kama walivyozungumzia waheshimiwa waliotangulia kwa kweli kiutendaji sio tu inaweza ikamharibia yeye kamishna kama bodi haitofanya vyema. Lakini pia yeye mwenyewe kamishna kwa sababu anatakiwa awajibike kwa bodi hawezi kuwa *part* ya ile bodi. Bodi kazi yake ni kuiangalia ile kamisheni inafanya kazi yake, sasa kama kutakuwa na mtendaji anatoka mle anaingia katika ile bodi ule usimamizi kidogo utakuwa na hitilafu.

Vile vile kama atakuwa ana *convincing language* huyu kamishna, basi vile vile kuna uwezekano mkubwa wa kui-*drag* ile bodi ikaenda na vile anavyotaka yeye. Sasa tungeomba Mhe. Waziri akaliangalia hili. Kamishna anaweza pale anapohitajika akaalikwa kwenye kikao kwa kutoa ufafanuzi wa masuala kama bodi itahitaji kufanyiwa hivyo, lakini asiwe *part and parcel* ya ile bodi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo mchango wangu mwengine niangalie zaidi kuhusu hii bodi madhumuni yake, uwezo wa bodi. Kwenye kazi ya bodi kifungu cha 6(c) kinazungumzia kwamba, bodi itapendekeza marekebisho katika sheria na kanuni zinazohusika na ukusanyaji wa mapato. Lakini ukiangalia katika kifungu hicho hicho cha 2 (h) nambari, kinasema kwamba Bodi ya Wakurugenzi haitokuwa na uwezo wa kuingilia kuhusu kiwango kinachopaswa kukusanywa na walipa kodi.

Sasa kwa mtazamo wangu mimi Mhe. Spika, naona kama hizi ni *contradictory ideas.* Hapa inasema kwamba wao ndio watakaokuwa washauri wakubwa katika suala zima la ukusanyaji, lakini pia kuna kifungu kwamba hawapaswi kuingilia. Sasa nikawa nina wasi wasi hapa isije ikawa *over looked* hii, tuangalie kama tumewapa hiyo *power board* basi kwa maana nyengine iwe na uwezo huo wa kuingilia. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia hili au akanifafanulia mimi labda sikuelewa vizuri, lakini kama ni hivi ilivyosomeka hapa basi zinaji-*contradict* Mhe. Spika.

Pia nimejaribu kuangalia pia mswada wenyewe ambao tumepatiwa hapa Mhe. Spika, haujazungumzia ni kwa kipindi gani vikao vitakuwa vinakutana vya

bodi, isipokuwa hapa imezungumzwa kwamba watakuwa wanakutana mikutano ya kawaida kwa ajili ya kupitia taarifa za mapato ya mwezi katika kila mwezi unaofuata wa makusanyo. Sasa mimi nikajiuliza, kwa sababu ninavyojua kila mwezi makusanyo yanafanyika, sasa hii bodi kila mwezi itakuwa inakaa? Kwa sababu haikuwekwa sawa. Nimeangalia na ule mswada wenyewe hasa pia hili halikuzungumzwa.

Mhe. Spika, kwa sababu kwa kawaida bodi huwa inapewa taratibu zake za kukutana kama kila baada ya miezi mitatu au minne wawe wanakaa, isipokuwa kama italazimika kuna suala muhimu linataka kupitishwa uamuzi wake na bodi basi kunakuwa na *extra ordinary board meeting*. Lakini sababu hii mimi sikuweza kuifahamu. Mhe. Waziri nitamuomba aje anifafanulie hili au kama sikuona basi ningeomba anielekeze kwamba bodi hii itakuwa na vikao vyake kwa utaratibu gain?

Lakini pia Mhe. Spika, nilipoangalia huu mswada wenyewe hasa ukurasa wa 7 kuna kipengele cha 9 kuhusu *delegation*, nafikiri *one delegate of power*. Hapa bodi wanasema kwamba, "*The delegate, may delegate to any member the power and authority to carry out on behalf of the board such functions as the board may determine, except powers given under sections 8(1)(f) and (1) of this act"*. Sasa mimi nikasema kwa nini wa-*delegate* hii *power* kwa *member? One member of the board why?*

Mhe. Spika, mimi nadhani utaratibu ni kwamba kuwe na kamati ndani ya bodi, wajumbe wa bodi waruhusiwe ile bodi kuwa na kamati ambayo ina wajumbe wa bodi ambao watafanya kazi kwa niaba ya bodi na sio mjumbe mmoja wa bodi.

Mhe. Spika huo ndio ulikuwa mtazamo wangu katika marekebisho haya madogo ambapo kama ulivyo mswada wenyewe ni mdogo, basi nimesema na mimi niwasilishe hapa ili Mhe. Waziri atakapokuja kutufafanulia atufafanulie. Vyenginevyo niungane na wenzangu kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Mimi binafsi lakini pia kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi ambao wao wameniwezesha mimi kuingia humu kuzungumza kwa niaba yao.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Naomba niwatangazie wale waheshimiwa walioko nje basi warudi ndani tumalize kazi. Nashukuru kwamba ile Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wamemaliza kazi kwa hivyo nategemea nao watarudi ndani ili tuendelee na shughuli hii.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya ya Bodi ya Mapato Zanzibar (Marekebisho) ya 2009.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka katika mawizara au mashirika mbali mbali kuweko na bodi za kusaidia mambo tofauti ya utendaji katika kazi zao, hii italeta ufanisi.

Mhe. Spika: Mhe. Thuwaybah E. Kissasi hutusubiri tukamaliza kazi hii? Basi nenda urudi haraka.

Mhe. Ali Denge Makame: Kuweko kwa bodi hizi kutasaidia mashirika au mawizara kuleta ufanisi wa mambo mbali mbali ya utendaji wa kazi zao. Mhe. Spika, haya si mageni kwa nchi kama yetu kuwepo na vitengo hivi katika mawizara. Kuna baadhi ya nchi mashirika au mawizara huwa yanaanzisha bodi ili kutaka kuleta fani zaidi katika utendaji wa kazi zao. Hivyo, utakuta nchi nyingi nyingi zina mfumo kama huu. Sasa na petu sisi kuwepo mfumo huu kutasaidia kupunguza baadhi ya mambo yanayohusiana na ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 50 kifungu cha 3, marekebisho ya kifungu cha 2, kuna maneno yamezungumzwa naomba kunukuu, "'Bodi ya Wakurugenzi' maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mapato Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha sheria mama".

Mhe. Spika, kwa muono wangu naona katika wizara hii kuanzisha bodi itakuwa ni utaratibu mzuri. Lakini ni vyema tusijaribu kuingiza na mfumo wa bodi nyengine, baada ya kuona Bodi ya Mapato halafu kukawa na bodi nyengine kama ya Wakurugenzi kutakuwa na mvutano. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anifafanulie vizuri zaidi ili maelezo haya nijue ni ufafanuzi wa bodi moja tu hii ya mapato au kuna bodi nyengine ya wakurugenzi ambayo itakuwa na nguvu zaidi zidi ya Bodi ya Mapato ambayo imeundwa hapa? Kwa hivyo, hili tu ningeomba aje anifafanulie vizuri niweze kulifahamu kwa kina zaidi.

Mhe. Spika, ukurasa wa 51 kuna maelezo yanayosema uwezo wa bodi.

Kifungu cha 6(1)(a)

> "Kuchukua hatua muwafaka za kuzuia ukwepaji wa kodi na uvujaji wa mapato ya serikali".

Mhe. Spika, kupewa uwezo bodi hii ni muhimu sana, kwa sababu kama inavyoeleweka katika ukusanyaji wa mapato kunakuwa na matatizo mengi

yanayowakuta wale wakusanyaji wa mapato yale. Kwa hivyo, pindi bodi hii ikipewa uwezo wa kuweka sheria ndogo ndogo au kanuni ili kumfanya yule mteja awe mwepesi wa kukusanya na kukubali taratibu za ukusanyaji wa mapato, basi itasaidia.

Katika ukusanya wa mapato kunakuwa na mbinu nyingi za uvujaji wa mapato na ukwepaji wa kulipa kodi, basi utakuta kama hakuna sheria ndogo ndogo za kuweza kumbana mtu anayekusanya mapato basi kutasababisha malengo yale tuliyoyakusudia yasifikie. Kama tunavyojua kuna baadhi ya watu kama wastaafu wa kazi kwa sehemu kama hizi wanakuwa wataalamu, sasa akishakuwa mtaalamu wa mambo kama haya mle mnamohusika kwenda kukusanya mapato akiwemo mtu yule huwa ni mtaalamu sana wa kutoa taaluma kwa yule anayelipa kodi ili kukwepesha mapato yale yasipatikane.

Kwa hivyo, ningeomba kitengo hiki cha Bodi ya Mapato kika wana wataalamu waliosomea na wenye uwezo wa kuzifikiria na kubuni mbinu mbali mbali za watu wa mapato wanaotaka kukwepesha ili wasizifanye.

Mhe. Spika, kama bodi hii itapewa uwezo wa kufanya hayo kwa wale wataalamu wachache wenye nia ya kukwepesha pamato haya huenda wasifanikiwe. Kwa hivyo, mimi kipengele hiki nakiunga mkono kiundiwe sheria na kanuni ili wapate kuitumia kwa kufanikisha masuala haya ya mapato.

Mhe. Spika, kama tutasimama kidete kuhakikisha ukusanyaji wa mapato haya na kuyapata kwa ukamilifu nafikiri baadhi ya malengo yetu mengi yatakwenda kwa mujibu wa sheria zile tulizozikusudia.

Jengine nije katika ukurasa wa 52 kifungu cha 8(b) kazi za Bodi ya Wakurugenzi zitakuwa kama ifutavyo: -

> Kusimamia bodi kwa mambo yanayohusika na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato chini ya sheria hii. Kama nilivyoeleza mwanzo maelezo yangu, katika kuunda bodi hii tuwe waangalifu sana ili ndani ya Wizara hii baada ya kwisha kuunda bodi moja basi tusifanye matokeo ya kuunda bodi nyengine ikawa ile bodi tuliyoikusudia kufanya kazi haina uhuru wa kufanya kazi zake kiukamilifu. Hapa ningemuomba Mhe. Waziri akafanya upembuzi wa kutosha ili kuhakikisha bodi hii tunayoiunda iwe inafanya kazi zake kwa mujibu wa mipangilio tuliyoikadiria.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu kama tutautekeleza kwa mujibu ulivyoandikwa humu na kufanya marekebisho mle mlimokuwa na

marekebisho, naona kutakuwa hakuna tatizo la kupata mapato yetu na makusanyo kwa mujibu wa kawaida na taratibu zetu tulizojiwekea.

Kwa hivyo, mimi mswada huu kama ulivyokwisha zungumzwa na baadhi ya wenzangu kuwa ni mswada mfupi na una maelezo mengi ambayo yanasomeka na kufahamika, basi nauunga mkono na tuendelee kuujadili vizuri na kuupitisha kwa lengo la maendeleo katika nchi yetu. Hivyo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja sina pingamizi nao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi naomba nichukue dakika chache sana nichangie mswada huu na niaze moja kwa moja kwenye marekebisho ya kifungu cha 8(1) Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba wenzangu wamezungumza juu ya nafasi ya Kamishna wa Bodi ya Mapato kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Lakini kwa mujibu wa uoni wao na wangu ni kwamba naunga mkono na mimi kuwa Kamishna wa Bodi ya Mapato asiwe mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Kwa sababu ukiangalia kazi zake, kazi za Bodi ya Wakurugenzi ni kwamba itamtaka Kamishna atoe taarifa na ripoti mbali mbali.

Sasa yeye atapokuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ni dhahiri kwamba taarifa hizi zinaweza zikawa finyu na ikawa hakuna utendaji na uwajibikaji. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba Kamishna wa Bodi ya Mapato kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ni kudhoofisha nguvu za Kamishna, lakini nadhani Bodi ya Wakurugenzi vile vile itakuwa haina uwezo kiasi hicho wa kumlazimisha mtendaji ambaye ni mjumbe wa sehemu ile.

Mhe. Spika, jengine ambalo nina wasi wasi nalo ni Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Tumekuwa na malalamiko makubwa juu ya Wazanzibari wanavyonyanyaswa ndani ya kodi na *TRA*, niseme hivyo. Sasa leo unamchukua mtu wa *TRA* unamuingiza ndani ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar ambapo Wazanzibari wana malalamiko na *TRA.* Kwa maoni yangu ni kwamba unamchukua mtu aje amege fedha zetu zaidi atukandamize.

Mhe. Spika, mimi mawazo yangu nasema kwamba, mtu wa *TRA* kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *ZRB* nadhani ni tatizo. Ni dhahidi kwa Wazanzibari sasa wanasogezwa kule ambako kilio chao kimekuwa cha muda mrefu. Kwa hivyo, mimi mawazo yangu ni kuwa mtu huyu tungesamehe na tukawaacha Wazanzibari wenyewe, wakurugenzi kutoka *ZRB* yenyewe, lakini msiwe na mtu wa *TRA* kwa sababu hata mipango ya njia za kodi *ZRB* itapanga njia zake za kukusanya mapato. Ni kusema kwamba njia zile za kukusanya mapato wanawapelekea haraka sana *TRA* waweze kuzijua.

Jengine ambalo naomba ufafanuzi kwenye kijifungu cha (f) ambapo waziri anaweza akateuwa si zaidi ya watu watatu, lakini mwisho kuna maneno kwamba wawe hawana maslahi binafsi katika bodi. Namuomba Mhe. Waziri akija hapa anifafanulie, hivyo kuna mtu gani aliyekuwa hana maslahi binafsi yuko kwenye bodi na huyo ndiye atakaefaa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi?

Mhe. Spika, jengine ningesema kuwa ni vyema mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ni mtu ambaye atateuliwa na Rais, lakini hatukusema huyu mtu awe na sifa gani. Sasa ni vyema katika nafasi kama hii tungesema mtu huyu pengine awe na kiwango gani cha elimu ili kumpa zaidi Mhe. Rais kuteuwa watu ambao wana sifa hiyo. Lakini kuweka wazi tu nina wasi wasi anaweza akateuliwa mtu hata hajui hiyo maana ya Bodi ya Wakurugenzi.

Mhe. Spaika, nasema kwamba ni vyeme tungesema Mwenyekiti wa bodi hii basi awe na kiwango fulani cha elimu , tena hapo unaweza ukampa Rais watu watano au sita akachagua mmoja mwenye sifa zaidi, lakini ukiacha wazi kama hivi nina wasi wasi anaweza akenda mtu ambaye hatoweza kuimudu kuiongoza Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wasi wasi wangu huo, niseme kuwa Mhe. Waziri anisaidie kwenye kamishna wa Bodi ya Mapato kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na huyu mtu wa *TRA* kuwa pia ni mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia wasaa huu wa kufanya majumuisho ya mswada wetu huu mdogo lakini muhimu sana kwa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 1996.

Mhe. Spika, najua waheshimiwa wangependa kuchangia zaidi lakini naamini wameuona mswada uko moja kwa moja hauna matatizo mengi. Kwa kweli nishukuru sana Kamati ya Fedha na Uchumi na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuipitia mswada huu na hata utaona makosa waliyobaini ni madogo mno. Najua Mhe. Spika, kule wana maprofesa wangu wengine huwa hawaridhiki kule juu bado na vipengele wanavileta na huku bondeni, lakini nashukuru na wao pia wameunga mkono hata huku bondeni hawakuzungumza. Kwa hivyo, hiyo ni imani yangu kwamba wameridhia marekebisho haya.
Mhe. Spika, naomba nitambue waheshimiwa waliopata fursa ya kuchangia mswada huu, jumla ni waheshimiwa wanane.

Naomba nianze kumpongeza :-

1. Mhe. Ali Abdalla Ali, Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi
2. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
3. Mhe. Ame Ussi Juma
4. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
5. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
6. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi
7. Mhe. Ali Denge Makame
8. Mhe. Hija Hassan Hija

Mhe. Spika, nawashukuru sana sana michango yao hii kama nilivyosema mswada ni mdogo lakini ni muhimu na michango yao niseme kwamba itatusaidia kuweka sawa zaidi yale mambo ambayo hayakuwemo. Lakini unajua tunapotafsiri kutoka *version* ya Kizungu kwenda Kiswahili huwa tunapata tabu kidogo kutafuta lile neno gani litumike wapi?

Tunao watu wanaotusaidia lakini bado utakuta pengine tafsiri sahihi huipati. Kwa hivyo, ningeomba sana Waheshimiwa wawe na ile ya mkononi, kwa sababu mwisho Mhe. Spika, akishamaliza kazi na hizi *chambers* anapelekewa Mhe. Rais kuweka saini basi inapelekwa ile ya Kizungu, ile ndio inayokaa moja kwa moja. kwa hivyo, nakubali kwamba kunaweza kuwa na maneno kidogo hayako sahihi kitafsisi, hilo tutazidi kupitia mpaka tupate ile *version* ya mwisho.

Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kweli kwenye mchango wake tunamshukuru sana ameunga mkono moja kwa moja kwa niaba ya kamati na jimbo lake, lakini pia amezidi kusisitiza umuhimu wa haya marekebisho tuliyoyafanya kwamba tuyazingatie na tuyasimamie ipasavyo. Nafikiri sisi tunakubali ushauri wake wote kwa niaba ya kamati na Mwenyewe amesisitiza kwamba hapana budi kwa kazi na uwezo unaokusudiwa kupewa Bodi ya Wakurugenzi utatoa mwelekeo mzuri wa mafanikio endapo tu utekelezaji wake utakuwa kama ulivyokusudiwa.

Kamati inaweka matumaini kwamba ipitapo sheria hii basi bodi hiyo itafanya kazi zake bila ya woga wala chuki na kwa uadilifu mkubwa. Hayo ndio mazingatio yetu na ndio matarajio yetu.

Kwa hiyo, namhakikishia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwamba bodi hii madhali tunaipa meno na

sio kama wanavyosema baadhi ya waheshimiwa kwamba haina meno. Kwa kweli tunaipa meno na tunazidi kuipa meno na ningekuombeni waheshimiwa mtusaidie. Hii si kazi ya bodi peke yake, ni kazi yetu sote, hili ni jukumu letu kama nilivyosema jana kwamba kodi ndio uhai wetu. Bado tunaambiwa kwamba zipo *avenue* nyingi za kodi inabidi tuzifuatilie tuzisimamie. Kama Mhe. Ame Ussi Juma alivyosema kwamba bado yapo maeneo, yapo mahoteli, zipo sehemu hatujazigusa hatujazifikia.

Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Ame Ussi Juma jana ameniandikia hasa hizo hoteli zinazofanya madudu kama haya. Kwa hiyo, tunachukua jukumu hilo tutazifuatilia kuona kwamba tunawawajibisha ipasavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji msemaji mkuu wa upinzani kwa masuala ya Fedha na Uchumi tunamshukuru sana na yeye kwa maoni yake na maelezo yake. Nithubutu kumwambia kwamba kwa kweli wizara na serikali tunakuwa makini sana wakati tunapofanya mabadiliko ya sheria. Niseme tu, unajua unapopanga ni jambo moja na unapotekeleza ni jambo jengine. Sasa unapotekeleza ndio unapoona yale matatizo na kuhusu sheria sasa inabidi u-*act* haraka sana kwa sababu usipo-*act* basi jamaa wanapata *loopholes* na kwa mfano kuhusu mapato tena unayakosa.

Kwa hiyo, inabidi usichoke kutusaidia Barazani kufanya haya marekebisho. Kwa sababu tusipofanya marekebisho kama nilivyosema *loophole* zipo na watu wana-*take advantage* mapato tunayakosa. Chukulia tu wewe ni *brain* moja una-*deal* na *brain* elfu na moja. Wewe unafikiri hivi, wao wana-*count up*, vipi wana-*count up* wa-*maximize* na wao yale mapato yao. Unajua siku zote mtu anachuma lakini hataki atumie isipokuwa a-*maximize* faida. Kwa hiyo, msione tabu kwamba tunaleta mara kwa mara tunazingatia.

Lakini kama anavyosema na wao wafanyabiashara, si wafanyabiashara tu, mtu yeyote nae anajipinda anaona vipi afanikishe jambo lake. Kwa hiyo, sisi tunajitahidi sana kuona vipi tunafanikisha.

Mhe. Spika, kama ninavyosema ile sheria utaitunga, madhali inaanza kutumika ndio unapoona yale matatizo, moja, mbili, tatu, sasa u-*act* haraka sana kuziba ule mwanya.

Mhe. Spika, namhakikishia Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwamba tunajipinda na tunafanya kazi pamoja. Hao wadau aliosema kama nilivyosema jana tuna kamati yetu ya *task force* ya *tax reform* na mara nyingi tunawaalika na hasa siku hizi hawa wafanyabiashara kwa sababu wao ndio walengwa. Tunawashukuru sana kwa sababu wangekuwa hawa-*comply* basi tusingefika hapa tulipo. Kwa kweli tumefika pahala pazuri sana na wanachangia vizuri

sana. Wengine tunao katika *section* zetu mbali mbali zile 7 nilizozitaja za makusanyo ya kodi tunafikia mpaka asilimia 100 au wengine wanapindukia. Hii inaonesha wazi jinsi wanavyo-*comply*.

Mhe. Spika, nitatoa mfano kwenye *motorvehicle registration* tumefikia mpaka asilimia 141 yaani tumepindukia hata lile lengo tulilotarajia. Sasa inaonesha wazi kwamba watu wame-*comply*. Labda nitoe mfano kwenye *road development fund* nako tumechangia mpaka asilimia 101. Kwenye *driving licence* asilimia 108, kila mmoja anaona umuhimu wake. Nazishukuru taasisi nyengine zinazohusika zinatusaidia. Kwa hiyo, hii yote inaonesha vipi tunavyoshirikiana taasisi zote kufanikisha suala zima la upatikanaji na ukusanyaji wa kodi.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji mbali ya hilo nakumbuka pia alizungumzia suala la Mwenyekiti kwamba *terms* zake labda tusioneshe kama upendeleo. Nafikiri sheria imeweka wazi kabisa na imesema kwa ufasaha kwamba Mhe. Rais atamteua Mwenyekiti wa Bodi na haukutajwa utaratibu wa kuweka mkomo wa muda wa Mwenyekiti kwa sababu unaweza ukaikosesha serikali fursa ya kumteua tena Mwenyekiti aliyefanya vizuri. Vile vile inaweza ikam-*limit* Rais kumuondoa endapo hakufanya vizuri. Kwa hiyo, tumeiweka wazi hii na hiyo ni *jurisdiction* ya Rais.

Mhe. Spika, humu kwenye sheria nafikiri imesema wazi wazi kwenye kifungu pale cha Mwenyekiti. Ukiangalia pale kwenye maelezo ya Uteuzi wa Mwenyekiti nafikiri tumeieleza kwa ufasaha kabisa naomba ninukuu kidogo.

Kifungu 8A (2):

> "Mwenyekiti ataitumikia ofisi kwa masharti na utaratibu kama itakavyoainishwa katika hati yake ya uteuzi kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu kwa muhula wa kwanza na anaweza kuteuliwa tena."

Kifungu 8A (3):

> "Rais anaweza kusitisha uteuzi wa Mwenyekiti kwa sababu ya kutoweza kutekeleza kazi zake, au kutokuwa na nidhamu, au kwa sababu nyengine yoyote ya msingi."

Nafikiri hizi ni *strong words* ambazo Rais akiona huyu Mwenyekiti wake hafanyi vizuri basi mara moja anaweza kumuondoa. Nafikiri hakuna wasi wasi wowote na kwa kweli Mhe. Rais tunaamini kabisa na washauri alionao hii kazi anaifanya vizuri na tunashukuru tunakwenda vizuri na matunda tumeyaona kwa

utendaji wa Bodi ya Mapato. Kwa hiyo, hili Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji nakuomba lisikutie wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala jengine ambalo Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na waheshimiwa wengi walilizungumza juu ya Kamishna kuwemo kwenye bodi. Nafikiri ni utaratibu wetu kwamba mara nyingi yule Mtendaji Mkuu wa taasisi yeye anakuwa ndio kama kiungo kwenye bodi. Haidhuru anakuwepo na Katibu wa Bodi lakini yule ndio kiungo kwenye ule utendaji wenyewe, *day to day running of the institution*. Sasa ukimuondoa kwenye bodi mara nyingi hupati ufanisi, si bodi hii tu lakini bodi nyingi tu, zote za Tanzania Bara hata zetu hapa Zanzibar utakuta tuna mfumo huo. Kwa kweli unaleta unafisi mzuri, *rather than* unaendesha vikao halafu hampati taarifa hii mtafute Mtendaji Mkuu au Mkurugenzi Mkuu aje atoe taarifa inakuwa hupati ile *flow* ya mambo unayoyataka ya bodi.

Lakini yule akiwemo ndani mle na yule sio Mwenyekiti, Mwenyekiti ndio mwenye mamlaka pale na bodi pale ndio imepewa meno na nini wafanye. Lakini pia ikiwa hawaridhiki basi wanaweza kumtoa nje wakamzungumza ipasavyo. Hiyo wenyewe wana taratibu zao bodi jinsi ya kumzungumza mtu hasa kwa Mtendaji Mkuu kama huyu. Kwa hiyo, naomba isiwape wasi wasi waheshimiwa wote walioichangia pointi hii, naamini hii imefanya makusudi kupata ile *flow* ya mtiririko wa kazi zetu.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji pia alipendekeza kwamba kuweko neno la uwajibikaji badala ya neno la ari. Nafikiri hii si mbaya sana, hii inakubalika na tutaizingatia fikra yako hasa ukitazama lile neno lililokusudiwa pale. Kwa sababu umetaja kwenye kifungu cha 4(c) *essence* yenyewe kwamba ni kuongeza ari ya kulipa kodi kwa hiari na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, nafikiri hiyo si tatizo tunaifikiria na vipi tunaweza tukaiweka.

Halafu Mhe. Spika, kulikuwa na suala la sekta binafsi uwakilishi wake. Nafikiri tumetoa nafasi moja, wewe ulisema kwa nini tusiongeze nafasi ya pili kama Kamisheni ya Utalii. Unajua hapa hasa kwa kwetu walipa kodi wengi ni wafanyabiashara na wao wanatoka sekta binafsi, sasa kuwapa nafasi nyingi kwenye bodi kidogo kuna matatizo yake. Tunajua wanalinda *interest* zao lakini kwenye bodi mle sisi tunataka kidogo wao wa-*comply*. Lakini sasa ukija pale tunazungumza maneno mengi na yule wakishakuwa zaidi ya mmoja kidogo kuna hatari. Kwa hiyo, tumehisi mjumbe mmoja anaweza kukidhi haja.

Lakini kama nilivyosema mara nyingi tunashirikiana nao, tunabadilishana mawazo nao na hatuamui mambo ambayo hayatekelezeki. Kwa hiyo, nafikiri haina athari sana.

Mhe. Spika, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji aliuliza kwamba kwa nini kuwe na maandishi ya mkono. Kilichokusudiwa ni kwa maandishi hata kama yatachapishwa kwa kompyuta ni maandishi yale ya mwenyewe Mhe. Waziri. Kwa sababu inaweza kutokea pengine mtu mwengine akaandika tu ikaonekana ni waziri, lakini yale maandishi yake hasa ndio iliyokusudiwa. Kama kidogo haikuleta maana nzuri kwa Kiswahili basi hiyo tutaipitia tuone vipi inaleta ile fikra tuliyoitaka.

Mhe. Spika, tunamshukuru Mhe. Ame Ussi Juma amezungumzia vizuri sana kwamba bodi iwe na meno. Kama nilivyosema tutajitahidi kuipa meno na iweze ku-*bite* ipasavyo.

Pia alizungumza kwamba kuna hoteli zinafanya kazi kodi hawalipi wanafanya ujanja ujanja huo. Nafikiri tutakuja kukaa nae pamoja atuongoze na hasa kwa vile jimbo lake lina mahoteli ya kitalii. Naamini atakuwa anayafahamu na atatusaidia sana na asiwe na wasi wasi hiyo tutakwenda *informal* na yeye tutamlinda. Si kwa yeye tu lakini hata Waheshimiwa Wawakilishi wengine kama wanazo taarifa hizi basi watushauri ipasavyo.

Mhe. Mzee Ali Ussi tunakushukuru kwa mchango wako kwa suala zima la utunzaji wa kumbukumbu. Umesisitiza umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu pia utolewaji wa risiti kwamba zitolewe na taasisi moja tu. Fikra hiyo tumeichukua na ndivyo tunavyofanya hivi sasa. Kwa kweli tunajitahidi risiti zote zichapishwe na zitolewe na Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Hazina. Tulikuwa tumegundua kuna ujanja tu wahasibu wetu baadhi yao kwa sababu wanaona tabu mara kwa mara kurudisha *return*, basi wana virisiti vyao vidogo vidogo utakuta hata *serial number* havina. Kwa hiyo, baadhi ya mapato huwa wanavitumia vile, mpaka yakishakuwa mengi ndio wanatumia zile risiti za serikali.

Mhe. Spika, kama alivyoshauri Mhe. Mzee Ali Ussi kwamba zitolewe risiti zinazotambulikana na taasisi moja tu kote, hilo tumelisikia na ushauri wako tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja nae tunamshukuru sana alizungumzia kazi za bodi na alizungumza kwamba kodi ya *income tax* na kuendeleza ujuzi wapewe *ZRB*. Jana tulizungumza suala la *income tax* na matatizo yake, lakini pia tunashukuru ulipotuongezea hili suala la kuendeleza ujuzi kodi hizi wapewe wao. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi hilo hakuna matatizo yoyote.

Mhe. Spika, halafu pia alizungumza kwenye kifungu cha 6 (2) (a) kwamba hukufahamu nini hasa kimekusudiwa. Ningekushauri tu labda pengine tafsiri

haikuwa nzuri, labda ipitie kidogo ya Kiingereza inasemaje nafikiri iko *straight forward* itakurahisishia muda itakuongoza. Kama baadae hujaifahamu vizuri tutabadilishana mawazo na wataalam.

Mhe. Spika, Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi tunamshukuru sana pointi yake moja ya Kamishna tumeipokea. Halafu alisema kwamba bodi kusimamia ukusanyaji wa mapato au kuingilia. Nafikiri wao ni wasimamizi wa shughuli nzima ya ukusanyaji wa mapato, lakini kwamba haitoingilia ile *day to day running of the institution* katika suala la ukusanyaji, hiyo si mantiki yenyewe iliyokusudiwa.

Mara nyingi bodi inakutana mwezi mara moja na wanakutana ku-*review* yale mapato yaliyokusanywa kwa mwezi lakini na utendaji wa kazi. Nafikiri sasa zimetolewa mpaka hadudi rejea zao kwenye mswada huu mpya na kwa hiyo ule mgongano na menejimenti hautokuwepo tena. Bodi ile ya Wakurugenzi itajua kazi zao zipi na wale menejimenti kazi zao zipi.

Maana katika taasisi nyingi kunakuwa na matatizo utakuta menejimenti wanagongana sana na Bodi ya Wakurugenzi kwa kusema wanaingiliana kazi zao, mwengine anataka hili, mwengine anataka lile.

Halafu alizungumzia suala la ku-*delegate powers* kwenye sheria, alisema kwenye ukurasa wa 7 para ya 9 nini hasa kimekusudiwa. "*The board may delegate to any member the power and authority to carry out on behalf of the board such functions as the board may determine, except powers given under section 8 (1) (f) and (1) of this act".*

Nafikiri hiyo sio kwamba ku-*delegate*, hawaziondoi kazi zao lakini wana-*delegate* kwa baadhi ya kazi. Kama walivyosema *"may delegate to any member the power and authority to carry out on behalf of the board such functions as the board may determine".* Kama labda watakavyohisi kwa wakati ule na hasa ilivyokusudiwa. Nafikiri kama ulivyosema ukiitafsiri utaipata maana yake lakini tunaweza kushauriana na wataalam zaidi wakatupa nini hasa wamekusudia.

Mhe. Ali Denge Makame tunakushukuru sana kwamba sheria ni marekebisho ya Bodi ya Mapato. Pia amesema upatikanaji wa wataalam tusimamie mafunzo nayo tumeyasikia. Lakini nataka kusisitiza zaidi kwamba Bodi ya Mapato ni taasisi ambayo imepewa jukumu la kusimamia sheria za ukusanyaji wa mapato ya serikali ambayo inaongozwa na Kamishna anayesimamia utekelezaji wa kazi za kila siku. Bodi ya Wakurugenzi ni chombo kinachosimamia utendaji wa taasisi *(ZRB)* katika kufanya kazi zake. Hiyo ndio tofauti hasa ya masuala haya mawili.

Mhe. Hija Hassan Hija tunakushukuru sana kwa mchango wako, suala la Kamishna nafikiri nimelijibu. Ulisema kwamba *TRA* kutoa mjumbe *ZRB*. Nafikiri siku zote tulivyokuwa tunahimiza kwamba taasisi hizi zishirikiane na nafikiri hii ndio moja ya mashirikiano. Waheshimiwa wengine walikuwa wanasema tuifanye *ZRB* wakala wa *TRA*, lakini tukasema kwa nini wawe wakala bora tuwape wao majukumu moja kwa moja.

Sasa kwa masuala ya kiutendaji tumehisi kwamba si vibaya kuwa na mjumbe kwa sababu ni taasisi ya kodi na kuna kodi za Muungano wanazikusanya. Kwa hiyo, katika chombo hiki cha *ZRB* nafikiri sio tatizo baya kwa ile *element* ya ushirikiano na kuleta ufanisi wa kodi na uzoefu. Lazima tukubali wenzetu hiki chombo chao kikubwa cha siku nyingi na wana wataalam wengi, hiki chetu kichanga lakini tunafanya kazi vizuri sana kwa mashirikiano.

Kwa hiyo, kwa kutokana na kuimarisha mashirikiano ni vyema Kamishna wa *TRA* Zanzibar ambaye anaitwa Naibu Kamishna kuwa Mjumbe wa *ZRB*. Aidha, hatua zinachukuliwa kurekebisha Sheria ya *TRA* kumuingiza Kamishna wa *ZRB* kuwa Mjumbe wa Bodi ya *TRA* kwa nafasi yake. Nao pia wenzetu huko wametupa nafasi katika bodi yao ya *TRA*, Kamishna wetu wa *ZRB* anaingia katika bodi ile

.

Sifa za Mwenyekiti wa Bodi. Katika bodi zote za wakurugenzi zilizoundwa hadi sasa hakuna sheria inayotaja sifa za kielimu kwa Mwenyekiti wa Bodi, mara nyingi unatumiwa uzoefu. Unaweza kutaja kielimu au kwa fani ile lakini hasa uzoefu. Kama nilivyosema tunamuachia mwenyewe Mhe. Rais *jurisdiction* yake naamini hatochagua mtu atakayemuangusha, atamchagua mtu pale atakayefanyakazi.

Siku zote lazima tutazame ule utendaji wa mtu anavyofanya. Basi ule utendaji wa mtu unaturidhisha kama nilivyosema mwanzo, hauridhishi yeye mwenyewe anajua na pengine kikimalizika kipindi cha wiki moja anambadilisha anaweka mwengine. Hivyo nafikiri ndio utaratibu unavyokwenda mote.

Kazungumza kuhusu suala la maslahi binafsi. Kwa kweli mimi silitarajii hilo kwa sababu bodi ni chombo cha ukusanyaji, hivyo ni vyema katika utendaji wake wajumbe maslahi wasiyaweke mbele katika chombo hiki ili kiweze kufanya kazi vizuri.

Unapozungumza bodi siku zote uchague wajumbe wasiwe *yes man* tu, waweze kwenda kule wakatoa hoja, waka-*challenge*, hiyo ndio *essence* hasa ya kuweka bodi. Lakini kwamba maslahi binafsi yakawa mbele utakuta bodi hiyo siku tatu tu na shirika utaliona *automatic* linasambaratika. Mimi nafikiri suala la maslahi hatutolizingatia katika uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi.

Mhe. Spika, kwa muhtasari nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii na niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao kwa kweli naamini itatusaidia.

Mhe. Spika, labda kulikuwa na suala la rehani nisije nikalisahau Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim aliuliza. Kweli rehani hapo nyuma tumeiondoa, lakini hasa kilichokusudiwa yaani kuweka mali isiyohamishika kama ni dhamana kwa ajili ya mkopo. Unajua ni neno la Kiswahili hilo, sio ile rehani hasa tuliyoikusudia ya huko nyuma.

Halafu Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi nilisahau kidogo anasema uwezo wa Bodi ya Wakurugenzi. Bodi ya Wakurugenzi ina uwezo wa kuweka na kusimamia sera za bodi kama taasisi pamoja na kusimamia uongozi na sio kusimamia kazi za utendaji wa kila siku.

Nafikiri vikao vya bodi nimezungumza na ile kukasimu madaraka kama nilivyosema nilielezea kwa ufupi tu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya kama nilivyosema nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na naomba tuupitishe mswada huu ili marekebisho haya yaweze kufanya kazi mara moja kwa lengo la kupata ufanisi katika bodi yetu hii ya *ZRB* na hatimae kupata mapato mengi kwa nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar ya Mwaka 1996

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili iweze kuupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar ya Mwaka 1996

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	-	Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu 2	-	Kusomwa

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1996

Kifungu 3	-	Marekebisho ya kifungu cha pili.
Kifungu 4	-	Marekebisho ya vifungu vya 5 na 6 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5	-	Marekebisho ya kifungu cha 8 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	-	Kuongeza vifungu vipya 8A, 8B na 8C pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar ya Mwaka 1996

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar ya Mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ilivyokuwa kazi za leo zimekamilika na muda wetu wa Baraza bado ungalipo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu uliahirishe mpaka kesho asubuhi tarehe 21/10/2009 saa 3:00 za asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kwa mashirikiano makubwa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 21/10/2009 saa 3:00 asubuhi)